DCB COMMERCIAL BANK

# DOKEZO LA HISA za Upendeleo



Hisa Moja (1) kwa kila Hisa Moja (1) iliyopo kwa bei ya Shilingi 110 kwa hisa

Idadi ya Hisa 97,646,913

Kiasi cha kukusanywa Shilingi 10,741,160,430

**Mshauri Kiongozi na Dalali Mdhamini**

iTrust FINANCE

## KALENDA YA MATUKIO MUHIMU




| | |
|---|---|
| Tarehe ya mwisho kununua Hisa | 5 Novemba 2024 |
| Tarehe ya Rekodi | 8 Novemba 2024 |
| Usambazaji wa Fomu kwa wanahisa | 11 Novemba 2024 |
| Kufungua Mauzo ya Hisa za Upendeleo | 11 Novemba 2024 |
| Kufunga Mauzo ya Hisa za Upendeleo | 6 Desemba 2024 |
| Tangazo la Matokeo ya Mauzo ya Hisa | 11 Desemba 2024 |
| Wasilisho la Rejesta kwa CSDR | 12 Desemba 2024 |
| Kuorodhesha kwa hisa DSE | 18 Desemba 2024 |

## TAARIFA YA ANGALIZO

Chapisho hili limeandaliwa kwa kuzingatia Kanuni za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana za mwaka 2000 zinazosimamia mitaji na Hisa za Upendeleo.

Nakala ya Chapisho hili imewasilishwa kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa ajili ya kuidhinishwa; na kwa Msajili wa Makampuni (BRELA) kwa ajili ya kusajiliwa.

Kuidhinishwa kwa chapisho hili na CMSA isichukuliwe kama kiashiria cha sifa za DCB Commercial Bank PLC au matumizi yake. Dhamana zilizotolewa katika chapisho hili hazijaidhinishwa wala kutoidhinishwa na CMSA.

Wawekezaji tarajiwa wanapaswa kuwa waangalifu kwenye mambo yote yaliyoelezwa kwenye kipengele kilichoandikwa "Viashiria vya Hatari" kwenye sehemu ya 5 ya chapisho hili.

Uwapo na mashaka yoyote juu ya yaliyomo kwenye chapisho hili, tafadhali wasiliana na mshauri wako mwelekezi wa mambo ya uwekezaji, wakala wa soko la hisa, mwanasheria, afisa wa benki au Mshauri mwelekezi wa mambo ya fedha.

## TAARIFA MUHIMU

Dokezo hili linatolewa na DCB Commercial Bank Plc (ambaye kwa kifupi atatambulikana kama "mtoaji" au "kampuni") na limeandaliwa kufuatia kutolewa na kuorodheshwa kwa hisa zinazotolewa chini ya zoezi la uongezaji mtaji wa DCB Commercial Bank Plc na hatimaye kuorodheshwa kwa hisa hizo mpya kwenye soko kuu la uwekezaji lililopo kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Hii ni kufuatia kupitishwa kwa azimio la Hisa za Upendeleo kulikofanywa na Bodi na Wanahisa kupitia makubaliano ya tarehe 14 Septemba 2024.

Fomu ya Maombi kwa ajili ya usajili wa Hisa za Upendeleo imeambatanishwa pamoja na dokezo hili. Zoezi la uuzwaji hisa litafunguliwa saa 3.00 asubuhi tarehe 11 November 2024 na kufungwa saa 10.00 jioni tarehe 6 Desemba 2024. Hatua za kufuatwa wakati wa kufanya maombi zimeainishwa kwenye sehemu ya pili ya dokezo hili na hata kwenye fomu yenyewe ya maombi.

Hisa zitakazoombwa, kutegemeana na maombi, zitapangwa kwa usawa kadri ya taratibu za utoaji hisa za DCB Commercial Bank Plc. Hisa hizo ndizo zitazingatiwa wakati wa ugawaji wa gawio kama itakavyotangazwa kwa mwaka wa fedha wa 2024 na kuendelea.

## TAARIFA ZA MTAZAMIO

Dokezo hili linajumuisha taarifa za matazamio yatokanayo na shughuli za kampuni. Taarifa zote, ukiondoa zile za kihistoria, zinapaswa kuchukuliwa kama taarifa za matazamio na zitajumuisha zile zinazohusu mikakati; maoteo ya uchumi; uwekezaji, mapato yatokanayo na soko, fedha, gharama, matarajio ya ukuaji, mtazamo wa shughuli za kampuni, kwa mtumishi mmoja mmoja au kampuni kwa ujumla; ukwasi, raslimali za mtaji, matumizi na matokeo yoyote kufuatia mashauri yoyote ya kisheria.

Taarifa hizi za matazamio hazina uhusiano na mambo ya kihistoria, bali zimezingatia maoni ya sasa kuhusu matokeo tarajiwa. Ndiyo maana taarifa hizi zinaongozwa na utumizi wa maneno kama “amini”, “inaweza”, “lenga”, “taraji”,”tegemea”, “tazamia”, “tabiri”, “uwezekano” “iliyopangwa” “kadiriwa” “tarajali” au mengine yanayofanana na hayo. Mfano wa Taarifa za Matazamio inajumuisha taarifa kuhusu msimamo ujao wa kifedha au faida tarajiwa, mtiririko wa kifedha, mkakati wa shirika, kiwango cha ukuaji, makadirio ya matumizi ya mtaji, mkakati wa manunuzi, mipango tarajiwa ya upanuzi wa miradi. Nyingine ni viwango tarajiwa vya matumizi ya mtaji, viwango vya ubadilishaji fedha, utabiri na vigezo vya mauzo, pamoja na vigezo vingine vya hali ya uchumi kama vilevi wango vya riba na mfumuko wa bei.

Mtoa dokezo anatoa tahadhali kwamba Taarifa ya Matazamio sio hakikisho la utendaji wa baadae. Matokeo halisi, hali ya kifedha na uendeshaji, ukwasi na maendeleo ndani ya sekta yanaweza kutofautiana na yale yaliyotarajiwa kwenye dokezo hili au kwenye taarifa ya matarajio.

Wawekezaji tarajiwa lazima wazingatie kwamba taarifa yoyote ya matarajio iloyopo kwenye dokezo hili, itahusika kwa tarehe tajwa tu. Ieleweke kwamba wakati flani, vigezo vipya vinavyoweza kusababisha kudorora kwa biashara ya DCB Commercial Bank Plc vinaweza kutokea na sio rahisi kuvitabiri na pengine kuvizuia.

Mtoa dokezo hawajibiki na hatarajii kufanya mabadiliko yoyote kwenye Taarifa ya Matarajio ndani ya dokezo hili baada ya kuchapishwa kwa dokezo hili, isipokuwa iwapo atalazimishwa kufanya hivyo kwa mujibu wa sharia.

## TAMKO LA BODI YA WAKURUGENZI

Bodi ya Wakurugenzi wa DCB Commercial Bank PLC, baada ya kujiridhisha inakubali kubeba wajibu wowote utakaotokana na kuchapishwa kwa dokezo hili. Mtoa dokezo amethibitisha kwa muithibati kwamba maelezo au uhusianisho wowote katika dokezo hili ni kweli na sahihi katika namna zote; na kwamba hakuna taarifa au maelezo yaliyoachwa kiasi cha kulifanya dokezo lote au sehemu yake kuwa batili au lenye kutoa taarifa za uongo.

Wakurugenzi wanatakiwa, kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 kutunza taarifa za kihasibu na wanawajibika kwa taarifa zote, ziwe za fedha, au nyingine zozote kama zilivyojumuishwa kwenye taarifa hii.

Wakurugenzi wanatambua kwamba wanawajibika kuweka mifumo ya ndani ya udhibiti wa fedha kama ilivyoanzishwa na kampuni, na wanapaswa kuweka mazingira sahihi wakati wote kuhakikisha kuna utangamano. Ili Wakurugenzi wafanikiwe kwenye hili, bodi ya wakurugenzi imeweka vigezo kadhaa vya ndani vinavyolenga kupunguza gharama na kuondoa uwezekano wa makosa au upotevu wa fedha.

Bodi ya Wakurugenzi wa DCB Commercial Bank PLC, ambao taarifa zao zinapatikana kwenye sehemu ya 4.5 ya dokezo hili, wanawajibika kwa pamoja na/au binafsi kwa yote kama ilivyoelezwa

| | | |
|---|---|---|
| Zawadia Nanyaro | Regina Mduma | 20 Septemba 2024 |
| **Mwenyekiti wa Bodi** | **Katibu wa Kampuni** | **Tarehe** |



## TAMKO LA MWENYEKITI

**Wapendwa Wanahisa,**

Kwanza kabisa, ningependa kutoa shukrani za dhati kwa kila mmoja wenu kwa msaada na ushiriki wenu thabiti katika Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika tarehe 14 Septemba 2024. Ninafurahi kutangaza kwamba idhini yenu ya Kutoa Haki ya Hisa katika Mkutano Mkuu uliopita ni hatua muhimu sana katika safari yetu ya kuboresha benki yetu na kuifanya iweze kuwa endelevu. Ninawahimiza sana wanahisa wote kutumia fursa hii na kujiandikisha kwa ajili ya kununua hisa hizi za upendeleo. kabla rejista haijafungwa tarehe 8 Novemba 2024.

Mwaka wa 2023, DCB ilionyesha uthabiti na uwezo wa kubadilika kuendana na mazingira ya kiuchumi na ya uendeshaji yaliyokuwa yakibadilika. Kama benki, tulifanikiwa kuongeza urari wa hesabu za benki yetu kwa 9%; uwiano wa wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi ilipungua kwa asilimia 50 kutoka asilimia 12 hadi 6 na mwenendo wa amana uliendelea kuwa chanya kwa mwaka mzima.

Zaidi ya hayo, Bodi ilifanya uamuzi wa kupitia nafasi muhimu za uongozi ambazo ni muhimu kwa kufikia mwelekeo wa kimkakati wa miaka 2024 - 2028. Mnamo 2023, Bodi iliidhinisha uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji mpya Bw. Sabasaba Moshingi ambaye ana uzoefu mkubwa wa zaidi ya miaka 30 katika sekta ya benki na ameonyesha uwezo mkubwa wa kubadilisha benki ndogo kuwa benki ya ngazi ya kwanza. Bw. Moshingi aliungana na benki mwishoni mwa mwaka 2023. Na uongozi wa sasa, Bodi ina imani kwamba maono ya kimkakati ya benki yataweza kutekelezwa ili kuongeza thamani kwa wanahisa.

Ili kuhakikisha uthabiti wa biashara kwa muda mrefu; Bodi na Uongozi wameandaa mkakati mpya wa miaka mitano kwa benki kuanzia 2024 hadi 2028. Maeneo muhimu ya mkakati ni pamoja na kuongeza mtaji wa benki hadi TZS 61 bilioni ifikapo 2028 na uwiano wa uwezo wa mtaji wa asilimia 19, mabadiliko ya mkakati wa kukusanya amana, ukuaji wa portfolia ya mikopo bora, kutoa huduma za benki kwa wafanyakazi wenye kipato cha chini na uboreshaji wa njia za utoaji huduma. Mkakati mpya wa miaka mitano utasababisha ukuaji wa usawa wa karibu nusu trilioni, ukuaji wa faida ya mtaji ya asilimia 21.8, na kufikia uwiano wa ufanisi wa gharama wa asilimia 48 pamoja na kudumisha viwango vya mikopo isiyolipika chini ya asilimia 4.5 ya benki.

Hivyo basi, Kutoa Hisa za upendeleo si tu kwa ajili ya kuongeza mtaji, bali ni hatua muhimu sana kuelekea kuimarisha mustakabali wa benki yetu. Tumeanzisha mkakati kamili wa kurekebisha na kubadilisha ambao, kwa msaada wenu, utatekelezwa kwa kasi kubwa. Kutoa Hisa za upendeleo kunawakilisha fursa ya pekee kwenu, wanahisa wetu wenye thamani, kuchangia na kunufaika na kupona kwa benki na mustakabali wetu pamoja.

Hivyo basi, tunapendekeza bei ya hisa ya Shilingi 110, ikionyesha ongezeko la asilimia 21.4 kutoka kwa bei ya wastani ya biashara, ambayo tunaamini ni sawa kulingana na mwenendo wa soko la sasa

Wakuruenzi wa Kampuni wanawajibika kwa ukamilifu na yote yaliyomo kwenye Dokezo hili. Tunaomba myatazame yote yaliyomo humu na kuyaelewa vizuri.

Ndimi,



Zawadia Nanyaro

**Mwenyekiti wa Bodi**

## YALIYOMO


**TAARIFA YA ANGALIZO** iii

**TAARIFA MUHIMU** iv

**TAARIFA ZA MTAZAMIO** v

**TAMKO LA BODI YA WAKURUGENZI** vi

**TAMKO LA MWENYEKITI** vii

**1. TAARIFA KUU KWA MUHTASARI** 1

1.1. Utangulizi 1

1.2. Ofa 1

1.3. Muhtasari wa taarifa muhimu kuhusu hisa za upendeleo 1

1.4. Lengo la Hisa za Upendeleo 1

1.5. Takwimu Msingi Nyingine za Hisa za Upendeleo 1

1.6. Ratiba ya Matukio Muhimu 2

1.7. Maelezo ya Kampuni Toaji 2

1.8. Washauri wa Muamala 3

1.9. Matumizi ya Mapato 3

**2. MAELEZO YA TANGAZO LA HISA ZA UPENDELEO** 4

2.1. Msingi wa Bei ya Ofa 4

2.2. Masharti ya Kutoa Haki ya Hisa 4

2.2.1. Vigezo Vya usajili 4

2.2.2. Uhamisho wa Haki 4

2.2.3. Hali ya Hisa Mpya 4

2.2.4. Tarehe ya kufungua na kufunga Hisa za Upendeleo 4

2.3. Sifa na haki kuhusu hisa 4

2.4. Wanahisa wenye sifa wanaweza kuchagua yafuatayo; 5

2.5. Hatua za kufuatwa kuhusu Hisa za Upendeleo kwa Wanahisa 5

2.6. Ada ya Maombi 5

2.7. Sera ya kukataa 5

2.8. Sera ya Kurejesha Fedha 6

2.9. Haki Zisizochukuliwa na Sera ya Mgawanyo 6

2.10. Wawekezaji wa Kigeni 6

2.11. Wajibu wa Kikodi 6

2.12. Gharama za Ofa 6

2.13. Sheria Inayosimamia 6

**3. TAARIFA ZA KAMPUNI TOAJI** 7

3.1. Historia 7

3.2. Maono 7

3.3. Mtazamo 7

3.4. Shughuli Kuu 7

3.5. Maoteo ya Uchumi 7

3.6. Mpango mkakati wa DCB: 7

3.7. Taarifa ya Fedha kwa kipindi cha miaka mitatu kinachoishia tarehe 31 Desemba 2023 8

3.8. Uwiano wa Meoneo Muhimu ya kiutendaji 8

3.9. Muhtasari Wa Kifedha Kwa Kipindi Cha Miaka Mitatu Kinachoishia 31 Desemba 2023 9
3.10. Muhtasari wa Makadirio ya Fedha 10
3.11. Mfumo wa Uendeshaji wa DCB 10
3.12. Orodha ya Wanahisa Wakuu Hadi kufikia Juni 2024 10
3.13. Bodi ya Wakurugenzi 10
3.14. Timu ya Uongozi 11
**4. UTAWALA WA KAMPUNI TOAJI 12**
4.1 Wajibu wa Bodi 12
4.2 Muundo wa Bodi 12
4.3 Bodi na kamati ya Uongozi 12
4.3.1 Kamati ya Bodi ya Ukaguzina Viashiria vya Hatari na ji 12
4.3.2 Kamati ya Bodi ya Utawala na Rasilimali Watu 12
4.3.3 Kamati ya Bodi ya Mikopo 13
4.4 Hisa za Wakurugenzi 13
4.5 Wasifu wa Bodi ya Wakurugenzi 13
4.6 Timu ya Uongozi 18
**5. VIASHIRIA VYA HATARI 22**
5.1 Vihatarishi Vinavyohusiana na Mtoaji wa Hisa 22
5.1.1 Vihatarishi fedha 22
5.1.2 Vihatarishi vya Uendeshaji 22
5.1.3 Vihatarishi vya Uzingatiaji Sheria 23
5.1.4 Vihatarishi vya Kimkakati 23
5.1.5 Vihatarishi Katika Sifa 23
5.2 Vihatarishi Vinavyohusiana na Masoko 23
5.2.1 Hatari ya Kiwango cha Riba 23
5.2.2 Hatari ya Fedha za Kigeni 24
5.2.3 Hatari za Kisiasa 24
5.3 Vihatarishi Vinavyohusiana na Hisa Zinazotolewa 24
5.3.1 Mabadiliko ya Bei ya Hisa 24
5.3.2 Hatari ya Kupungua kwa Asilimia ya Umiliki wa Hisa 24
**6. TAARIFA ZA KISHERIA 25**
6.1. Maelezo Juu ya Usajili 25
6.2. Ofisi za Kampuni toaji 25
6.3. Mtaji wa Hisa Ulioidhinishwa na Kutolewa 25
6.4. Sera ya Gawio 25
**7. RIPOTI YA MHASIBU 26**
**8. FOMU YA MAOMBI 30**

# DOKEZO LA HISA za Upendeleo



# 1. TAARIFA KUU KWA MUHTASARI

## 1.1. Utangulizi

Sehemu hii inajumuisha ufupisho wa ofa kwa ajili ya Hisa Mpya. Dokezo hili lapaswa kusomwa lote pamoja na makabrasha mengine yaliyotolewa ili kupata picha halisi ya ofa.

## 1.2. Ofa

DCB Commercial Bank PLC imetoa kiasi cha hisa mpya zipatazo 97,646,913 kwa Shilingi 110/= kwa kila hisa ili kukusanya Shilingi 10,741,160,430/= (kabla ya ada) kwa kutumia dokezo hili kwa mgawanyo wa hisa moja kwenye kila hisa anayomiliki mwanahisa mpaka kufikia wakati rejista itakapofungwa tarehe 08 Novemba 2024.

## 1.3. Muhtasari wa taarifa muhimu kuhusu hisa za upendeleo

| | |
|---|---|
| Bei ya Ofa | Shilingi 110 kwa hisa |
| Idadi ya hisa zinazotolewa | Hisa 97,646,913 |
| Mtaji uliokusudiwa kukusanywa kwa | Shilingi 10,741,160,430 |
| Uwiano wa hisa za upendeleo | Hisa 1 mpya kwa kila hisa 1 iliyopo |

## 1.4. Lengo la Hisa za Upendeleo

Kutoa hisa za upendeleo kunafanyika kufuatia azimio lililofanywa na Bodi ya Wakurugenzi ya DCB na kuidhinishwa katika Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika tarehe 14 Septemba 2024. Mapato yatakayopatikana kutokana na Kutoa Haki ya Hisa yatatumika kwa:

- Kukusanya kiasi kikubwa cha mtaji wa hisa ili kufadhili ukuaji wa benki kama ilivyoainishwa katika mpango mkakati wa miaka mitano.Strengthening the balance sheet of the bank.
- Kuhakikisha uimara wa usawa wa benki.

## 1.5. Takwimu Msingi Nyingine za Hisa za Upendeleo

| | |
|---|---|
| Thamani halisi ya kila hisa | Shilingi 250 |
| Jumla ya hisa zilizoidhinishwa na DCB Commercial PLC | 400,000,000 |
| Jumla ya hisa zilizotolewa na kulipwa kabla ya Hisa za Upendeleo | 97,646,913 |
| Mtaji wa hisa ulioidhinishwa na DCB Commercial Bank PLC | Shilingi 100,000,000,000 |
| Mtaji hisa wa DCB Commercial Bank PLC kabla ya kuchapishwa kwa Hisa za Upendeleo (Hisa 97,646,913) | Shilingi 24,061,904,000 |
| Mtaji wa Soko (bei ya kufungia ilikua Shilingi 140 kwenye soko la hisa la Dar es Salaam 31 Agosti 2024) | Shilingi 13,670,567,820 |
| Bei ya ofa kwa hisa moja | Shilingi 110 |
| Idadi ya hisa mpya za Upendeleo | 97,646,913 |
| Idadi kamili ya hisa zilizotolewa na kulipwa baada ya Hisa za Upendeleo | 195,293,826 |

### 1.6. Ratiba ya Matukio Muhimu

| Tukio | Tarehe |
|---|---|
| Tarehe ya mwisho kununua Hisa | 5 Novemba 2024 |
| Tarehe ya Rekodi | 8 Novemba 2024 |
| Usambazaji wa Fomu kwa wanahisa | 11 Novemba 2024 |
| Kufungua Mauzo ya Hisa za Upendeleo | 11 Novemba 2024 |
| Kufunga Mauzo ya Hisa za Upendeleo | 6 Desemba 2024 |
| Tangazo la Matokeo ya Mauzo ya Hisa | 11 Desemba 2024 |
| Kuwasilisha Rejista kwa CSDR | 12 Desemba 2024 |
| Kuorodheshwa kwa Hisa DSE | 18 Desemba 2024 |

### 1.7. Maelezo ya Kampuni Toaji

| | |
|---|---|
| i) Jina | DCB Commercial Bank PLC |
| ii) Jina la Ofisi kadri ya usajili | DCB House, Plot No. 182 Block R<br>Morogoro Road<br>S.L.P 19798<br>Dar es Salaam, Tanzania<br>Simu: +255-22-2172201<br>Barua pepe: info@dcb.co.tz |
| iii) Afisa Mtendaji Mkuu | Bw. Sabasaba Moshingi |
| iv) Benki Kuu | Bank of Tanzania<br>S.L.P 2939<br>Dar es Salaam |
| v) Wakaguzi wa Nje | KPMG East Africa<br>The Luminary, 2nd Floor<br>Haile Selassie Road, Masaki<br>Dar es Salaam<br>Simu: +255-67-422-003/656-264-800 |
| vi) Kalenda ya Fedha | 31 Desemba |

### 1.7. Washauri wa Muamala

| | |
|---|---|
| Mshauri Kiongozi | iTrust Finance Limited<br>429 Mahando Street, Block C, Masaki<br>S.L.P 22636,<br>Dar es Salaam, Tanzania |
| Benki Pokeaji | DCB House, Plot No. 182 Block R<br>Morogoro Road,<br>S.L.P 19798,<br>Dar es Salaam, Tanzania |
| Wakala Mdhamini | iTrust Finance Limited<br>429 Mahando Street, Block C, Masaki<br>S.L.P 22636,<br>Dar es Salaam, Tanzania |
| Mshauri wa Kisheria | Endoxa Law<br>15 Tunisia Road,<br>S.L.P 19798,<br>Dar es Salaam, Tanzania |
| Mhasibu Taarifu | Auditax International<br>Auditax House,<br>S.L.P 77949<br>3rd Floor, Coca-Cola Road. Dar es Salaam, Tanzania. |
| Msajili | CSD & Registry Company Limited,<br>2nd Floor, Kambarage House,<br>6 Ufukoni Street.<br>S.L.P 70081,<br>Dar es Salaam, Tanzania. |

### 1.8. Matumizi ya Mapato

Mapato halisi yatakayopatikana kutokana na tangazo la Hisa za Upendeleo, yatatumika kwa ajili ya;

- kufadhili ukuaji wa benki kama ilivyoainishwa katika mpango mkakati wa miaka mitano.
- Kuhakikisha uimara wa usawa wa benki.

## 2. MAELEZO YA TANGAZO LA HISA ZA UPENDELEO

### 2.1. Msingi wa Bei ya Ofa

Wakurugenzi wameweka bei ya Kutoa Hisa za Upendeleo kuwa Shilingi 110 kwa kila hisa, ikiwa ni punguzo la takriban asilimia 21.4 kutoka kwa bei ya soko ya Shilingi 140 katika soko la hisa la Dar es Salaam kufikia tarehe 31 Agosti 2024.

### 2.2. Masharti ya Kutoa Haki ya Hisa

#### 2.2.1. Vigezo Vya usajili

Waombaji watatakiwa kuzingatia masharti na vigezo vifuatavyo;

1. Ofa hii haitawahusu wote wasio kuwa na sifa za wanahisa mpaka kufikia tarehe ya rekodi.
2. Hisa za Upendeleo kwa wanahisa ni kwa uwiano wa hisa moja kwa kila hisa moja ya msingi.
3. Idadi ya hisa mpya kwa kila mwanahisa mwenye sifa ni kama ilivyoainishwa kwenye dokezo Dokezo litapatikana kwa wanahisa kupitia njia za kielektroniki na nakala za karatasi zitapatikana pia katika matawi yote ya DCB, ofisi zote za mawakala wa soko la hisa na ofisi za DCB.
4. Wanahisa wenye sifa, wana uhuru, wakipenda, wa kutochukua hatua yoyote; na uamuzi huo utachukuliwa kama inavyoneshwa kwenye 5 na 6 hapa chini.
5. Wanahisa wenye sifa na ambao tayari wamenufaika na stahiki zao, wana haki pia ya kuomba kununua hisa ambazo hazikupata wanunuzi. Wanahisa waliostahili watalazimika kuonesha idadi ya hisa za ziada katika fomu ya maombi. Baada ya kufungwa kwa zoezi hili, hisa zozote ambazo hazitachukuliwa zitagawiwa kwa wanahisa ambao waliomba kuchukua hisa zaidi katika fomu zao za maombi.
6. Hisa baki zozote, baada ya namba 5 hapo juu, zitatwaliwa na “underwriting consortium” gharama ya Shilingi 110 kwa kila hisa kadiri ya masharti yaliyoainishwa kwenye mkataba wa uthibitisho.

#### 2.2.2. Uhamisho wa Haki

Kwa mujibu wa uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya DCB Commercial Bank PLC na Mkutano Mkuu wa Mwaka, haki hizi zitakuwa kwa wanahisa wa sasa pekee na hazitahamishika.

#### 2.2.3. Hali ya Hisa Mpya

Hisa Mpya zitapangwa kwa usawa (pari passu) kwa kuzingatia vigezo vyote kwenye mchanganuo wa hisa endelevu za DCB Commercial Bank Plc. Hii itajumuisha haki ya kupokea kwa ukamilifu gawio na mgawanyo mwingine wowote kadri itakavyotangazwa, kwa mwaka wa fedha unaomalizikia tarehe 31 Desemba 2024.

Wanahisa wenye sifa na watakaokuwa wamekamilisha hatua za kukubali kama zilivyoainishwa kwenye dokezo hili, watapokea hisa zao kwa njia ya kielektroniki katika namna ya krediti kupitia akaunti zao za CDS. Ni wajibu wa mwanahisa mwenyewe kuhakikisha kwamba taarifa zake za akaunti ya CDS ni kama zilivyoainishwa kwenye fomu ya ustahili na ile ya kukubali umiliki wa hisa.

Hisa mpya zitaingizwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) siku ya Ijumaa tarehe 18 Desemba 2024 huku mauzo yakianza siku hiyohiyo.

#### 2.2.4. Tarehe ya kufungua na kufunga Hisa za Upendeleo

Haki ya wanahisa kuwa wa kwanza kununua hisa mpya itakuwa kuanzia saa tatu kamili jumatatu asubuhi tarehe 11 Novemba 2024 na itafungwa saa 10:00 kamili jioni siku ya Ijumaa tarehe 6 Desemba 2024.

### 2.3. Sifa na haki kuhusu hisa

Ustahili wa mwanahisa umeoneshwa kwenye Fomu Ya Maombi. Idadi ya hisa mpya zitakazotolewa kwa wanahisa wanaostahili imepangwa katika namna ya fidia kutegemeana na wastani wa hisa zinazomilikiwa.

**2.4. Wanahisa wenye sifa wanaweza kuchagua yafuatayo;**

i) Kukubali kwa ukamilifu: Mwanahisa anaweza kuamua kuchukua hisa zake zote stahiki:

ii) Kukubali kwa sehemu: Mwanahisa anaweza kuamua kulipia hisa chache tu na zinazobaki zitahesabiwa kwamba hazikununuliwa.

iii) Kutofanya lolote: Mwanahisa anaweza kuamua kutofanya lolote na hivyo haki yake ya kupata hisa itakuwa imeondoka.

**2.5. Hatua za kufuatwa kuhusu Hisa za Upendeleo kwa Wanahisa**

i) Pale ofa inapokubaliwa, haiwezi kukataliwa tena.

ii) Wote wanaotaka kuomba hisa mpya, watalazimika kujaza fomu na Kukubalika.

iii) DCB Commercial Bank Plc au washauri wake, mawakala walioidhinishwa, mtoa Dokezo au wakala wake hawatawajibika kwa lolote pale ambapo Fomu ya maombi haikupokelewa mpaka tarehe ya mwisho, ispokuwa tu iwapo jambo hilo limetokea kwa sababu ya uzembe.

iv) Kukubali kunaweza kufanywa kwa kupitia fomu ya maombi iliyojazwa kikamilifu na ikatumwa kwa njia ya mtandao; au iliyowasilishwa kwa njia ya mkono pamoja na ada ya maombi ambayo itategemea kiwango cha hisa kinachoombwa. Kiasi hicho hakiwezi kurudishwa na kitathibitisha uhalali wa maombi ya hisa mpya kama itakavyokuwa imeelezwa kwenye fomu husika

v) Ikishajazwa, fomu ya maombi lazima irudishwe DCB Commercial Bank Plc moja kwa moja au kupitia wakala aliyeidhinishwa. Fomu hiyo itapaswa kuambatana na uthibitisho wa malipo kulingana na hisa zinazoombwa. Malipo ya ada ya maombi lazima yafuate utaratibu kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 2.7 sio zaidi ya saa 10.00 jioni siku ya Ijumaa ya tarehe 6 Desemba 2024.

vi) Maombi yote yanapaswa kuwasilishwa ndani ya muda kama ulivyotajwa hapo juu. Ni muhimu kuzingatia kwamba, maombi yote ya hisa mpya yatakayopokelewa na DCB Commercial Bank Plc au Wakala aliyeidhinishwa, nje ya tarehe zilizooneshwa kwenye dokezo hili, hayatasajiliwa.

vii) Wanahisa wenye sifa na ambao wangependa kuchukua stahiki zao, watapaswa kujaza kipengele cha “Kukubali kwa Ukamilifu” pamoja na vipengele vingine husika vilivyo kwenye Fomu ya Maombi. Wanahisa wenye sifa wanaotaka kupokea sehemu tu ya stahiki zao, watapaswa kujaza kwenye Fomu ya maombi Sehemu iliyoandikwa “Kukubali kwa Sehemu” pamoja na vipengele vingine husika vilivyo kwenye Fomu ya maombi.

viii) Wanaoruhusiwa kufanya maombi ni wanahisa wenye sifa tu.

**2.6. Ada ya Maombi**

Malipo ya hisa mpya yaliyo chini ya shilingi milioni tano yatafanywa kupitia benki au mitandao ya simu; au kupitia TISS kwa hisa zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni tano. Miamala yote inapaswa kuwa kwa shilingi za Kitanzania na ifanywe kwenye akaunti ya benki iliyooneshwa kwenye dokezo hili na kwenye fomu husika.

Malipo yanaweza pia kufanywa na mwanahisa moja kwa moja kwa kuweka fedha kwenye akaunti ya malipo. Ifahamike kwamba hakutakuwa na riba yoyote itakayolipwa na DCB Commercial Bank Plc kwa pesa zilizopokelewa.

**2.7. Sera ya kukataa**

Licha ya utaratibu wa kukubalika uliowekwa chini ya kifungu cha 2.5, ni uamuzi wa Wakurugenzi wa DCB Commercial Bank Plc na kwa ruhusa ya CMSA maombi yanaweza pia kukataliwa kwa sababu zifuatazo:

a) Iwapo fomu ya maombi inakosekana;.

b) Iwapo fomu haina namba ya CDS;

c) Kukosekana kwa jina la mwombaji mkuu/waombaji/jina la kampuni ombaji kwenye maombi yoyote;

d) Kukosekana au kuwapo kwa namba ya utambulisho iliyokosewa, ikiwemo namba ya utambulisho wa kampuni;

e) Kukosekana kwa namba ya akaunti;

f) Hati za utambulisho zisizokidhi;

g) Kukosekana kwa maelezo ya kampuni;

h) Kukosekana kwa Fomu ya Maombi au iliyopo kuwa imesainiwa kwa njia isiyofaa.

### 2.8. Sera ya Kurejesha Fedha

Hakutakuwa na riba itakayolipwa kwa mwanahisa mwenye sifa au mtu mwingine yeyote anayestahili, kwa ada yoyote ya maombi. Ikiwa hisa ambazo hazijachukuliwa zimesajiliwa na wanahisa waliopo, basi baada ya mgao sawia kwa kila mmoja, marejesho yatalipwa kwenye akaunti ya Benki iliyotolewa katika Fomu ya Maombi.

### 1.9. Haki Zisizochukuliwa na Sera ya Mgawanyo

Wanahisa wote wenye sifa watakaoomba Hisa Mpya kwa ukamilifu watapokea idadi kamili ya Hisa Mpya kama zilivyooneshwa katika Fomu ya maombi zao. Hisa Mpya ambazo hazijachukuliwa zitakuwa Haki Zisizochukuliwa ambazo zitauzwa kwa wanahisa wanaostahiki ambao wameziomba kwa Shilingi 110 kwa kila hisa na hisa zozote zilizosalia ambazo hazijachukuliwa zitachukuliwa na Wathibitishaji kwa bei sawa na masharti yaliyotolewa katika mkataba wa makubaliano.

### 2.10. Wawekezaji wa Kigeni

Wawekezaji wa Kigeni wenye sifa na wanaotaka kutuma maombi lazima wajiridhishe na uzingatiaji kamili wa sheria za mamlaka husika na ridhaa za serikali na nyinginezo ili kuhakikisha kwamba taratibu zote zinazohitajika zinafuatwa, na kuhakikisha kwamba wamelipa na kutuma kodi zote zinazotozwa katika mamlaka husika kadiri ya taratibu zilizopo.

Kabla ya kutuma maombi na hatimaye kununua Hisa Mpya, wawekezaji wa kigeni wanashauriwa kupata ushauri wa kitaalamu toka kwa washauri wao wenyewe iwapo wanahitaji idhini yoyote ya serikali au mamlaka nyinginezo na iwapo wanahitaji kuzingatia mahitaji yoyote ya kisheria au udhibiti.

Wanahisa wa Kigeni wenye sifa wanaombwa kuzingatia kwamba DCB Commercial Bank Plc iko chini ya masharti ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania na Kanuni husika zilizowekwa chini yake.

### 2.11. Wajibu wa Kikodi

Wanahisa wenye sifa wanaoguswa na kutaka kushiriki katika Hisa za Upendeleo ya kwanza kwa wanahisa, wanapaswa kushauriana na washauri wao wa kodi kuhusu athari au wajibu wowote wa kikodi unaoendana na Suala la Haki. DCB Commercial Bank Plc na Wakurugenzi wanaona kuwa si sahihi kwa wao kutoa ushauri wa kina kuhusiana na matokeo ya kodi kuhusiana na Suala la Haki isipokuwa kwa yale yaliyoainishwa katika Dokezo hili.

### 2.12. Gharama za Ofa

| Role | Kiasi (SHILINGI) |
|---|---:|
| Malipo ya Washauri | 240,000,000 |
| Malipo ya Uhakikisho wa Ununuzi wa Hisa | 150,000,000 |
| Ada za Tathmini ya Dokezo ya CMSA | 50,289,430 |
| Ada za Uorodheshaji DSE | 30,000,000 |
| Gharama za Uchapishaji | 15,000,000 |
| Masoko na Uhamasishaji | 25,000,000 |
| Ada za Mawakala wa soko la Hisa (0.6%) | 70,305,790 |
| Gharama nyinginezo | 30,000,000 |
| Ada ya CSDR | 10,000,000 |
| **Jumla ya Gharama za Utoaji Hisa** | **620,595,220** |

NB.

*Takwimu hizi hazijumuishi VAT (panapohusika) na zinaweza kubadilika.

### 2.13. Sheria Inayosimamia

Dokezo hili na mkataba wowote utakaotokana na kukubaliwa kwa ombi la kununua Hisa Mpya zitasimamiwa na kufafanuliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

## 3. TAARIFA ZA KAMPUNI TOAJI

### 3.1. Historia

Benki ya DCB ni benki ya biashara nchini Tanzania. Benki inatoa huduma za kibenki kwa watu binafsi, biashara ndogo na za kati, pamoja na wateja wakubwa wa mashirika. DCB Bank ina mtandao wa matawi 9, zaidi ya mawakala 700, na ni mwanachama wa zaidi ya ATM 280 za Umoja Switch.

DCB ilisajiliwa kama kampuni tarehe 6 Septemba 2001. Mnamo Aprili 2002, DCB ilianza biashara kama taasisi ya kifedha ya kanda. Tarehe 12 Juni 2003, benki ilipewa leseni ya kufanya biashara ya kibenki kama Dar es Salaam Community Bank Limited.

Mwaka 2008, DCB ikawa benki ya kwanza nchini Tanzania kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Mnamo Februari 2012, benki ilipewa leseni ya kufanya biashara ya kibenki kote nchini kama benki kamili ya biashara. Benki ilibadilisha jina kutoka Dar es Salaam Community Bank Plc hadi DCB Commercial Bank Plc.

### 3.2. Maono

Dira ya DCB Commercial Bank Plc ni kuwa mtoa huduma wa kifedha anayependekezwa zaidi nchini Tanzania

### 3.3. Mtazamo

Kutoa huduma za kifedha zinazofaa, bora, na bunifu kwa wateja wetu wapendwa, huku tukichangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuzalisha thamani kwa wanahisa.

### 3.4. Shughuli Kuu

Shughuli kuu za Benki ni kupokea amana kwa mahitaji, kutoa mikopo ya muda mfupi, wa kati, na wa muda mrefu, pamoja na huduma zingine za kibenki zinazoruhusiwa chini ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006. Sehemu kuu za biashara ni Watu Binafsi, Mikopo ya Vikundi, na wateja wakubwa wa kibiashara.

### 3.5. Maoteo ya Uchumi

Mtazamo wa jumla wa utendaji wa jumla wa uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa thabiti, huku Pato la Taifa (GDP) likiongezeka hadi kufikia asilimia 5.2 mwaka 2023 (ikilinganiushwa na 5.7%: 2022). Ukuaji wa Pato la Taifa unatarajiwa kuongezeka katika mwenendowa ukuaji wake wa sasa wa hadi kufikia wastani wa karibu 7% kwa mwaka.

Matarajio chanya yanatarajiwa kutokana na uwekezaji kimkakati unaoendelea katika sekta ya miundombinu hususan barabara, reli na uwekezaji unaoimarisha ukuaji kwenye uzalishaji wa umeme nchini, ambavyo vinatarajiwa kuongeza uzalishaji wa ndani.

Vichocheo vikuu vya ukuaji wa Pato la Taifa ni kilimo, mawasiliano, usafirishaji, mwingiliano wa kifedha, uzalishaji viwandani, ujenzi, na sekta za biashara za rejareja. Kiwango cha mfumuko wa bei kimebaki thabiti chini ya asilimia 5 kwa miaka michache iliyopita hata licha ya mitikisiko mikubwa ya kimataifa katika minyororo ya ugavi

### 3.6. Mpango mkakati wa DCB:

- **Ukuaji wa Mtaji** - Uchangiaji wa mtaji kupitia kutoa hisa za haki utaiwezesha benki kuongeza uwezo wake wa kutoa mikopo, kuwekeza katika teknolojia za kisasa, na kuboresha utoaji wa huduma katika njia zake zote. Zaidi ya kutoa hisa za haki, benki inaendelea kuchunguza njia za ziada za kuimarisha mtaji wake. Hii inajumuisha kutoa hati fungani za kampuni ili kuvutia uwekezaji wa muda mrefu na ushirikiano wa kimkakati na wakopeshaji wa ndani na wa kimataifa. Miradi hii inalenga hasa katika kusaidia wanawake, vijana, na kukuza uendelevu wa mazingira.
- **Ukuaji wa Amana za Wateja –** Mkakati wa ukuaji wa amana za benki unalenga kuongeza uwiano wa amana nafuu ikilinganishwa na amana ghali kutoka mchanganyiko wa sasa wa 30:70 hadi 40:60 ifikapo 2028. Hii itafanikiwa kupitia mipango iliyolengwa kwa sehemu kuu za amana. Benki itaimarisha uhusiano wake na wanahisa wake wakuu, hususan mamlaka za serikali za mitaa za Dar es Salaam, ili kuelekeza biashara zao kwa Benki ya DCB.
- **Uboreshaji wa Njia za Huduma** – Benki inapanga kuboresha mtandao wake wa matawi pamoja na njia zake za kidijitali. Benki inapanga kufungua matawi mapya sita (6) na kuhamisha matawi matatu (3) yaliyopo kwenda maeneo ya kibiashara yenye mikakati bora zaidi. Upanuzi huu utaongeza uwepo wa kimwili wa benki na kufanya huduma zake kupatikana kwa wateja wengi zaidi. Safari ya mabadiliko ya kidijitali itaendelea kwa maboresho ya USSD, programu za simu, benki za mtandao, na majukwaa ya mawakala. Maboresho haya yamelenga kuboresha uzoefu wa wateja na kuhakikisha kuwa njia za kidijitali zinaweza kushughulikia ongezeko la miamala kwa ufanisi.

- **Ukuaji wa Mali Bora na Utofauti wa Mapato** - Benki inalenga kukuza mkopo wake kutoka Shilingi bilioni 120 hadi Shilingi bilioni 332 ifikapo 2028, wakati huo huo kuongeza vyanzo vya mapato yasiyotokana na ufadhili. Hii itafanikiwa kwa kuboresha njia mbadala, bima kupitia benki, fedha za biashara, na miamala ya hazina. Benki inalenga kuongeza asilimia ya wateja wanaotumia huduma za kidijitali kutoka asilimia 32.5 hadi asilimia 45.0, ili kuongeza ushirikishwaji wa wateja na kizazi cha mapato. Mkopo wa mikopo midogo (microcredit) unatarajiwa kukua hadi Shilingi bilioni 50, wakati mikopo ya kibiashara inakadiriwa kukua hadi Shilingi bilioni 186.
- **Huduma za Kibenki kwa Wenye Kipato Kidogo (Mikopo Midogo na MSME**) - Kutambua uwezo katika sehemu ya kipato cha chini, benki itaongeza mkazo wake katika mikopo midogo na benki za MSME. Kwa kupanua huduma za kifedha kwa sehemu ambazo hazijapata huduma za kutosha, benki inalenga kuchangia katika ujumuishaji wa kifedha huku ikifaidika na soko lenye ukuaji mkubwa.


### 3.7. Taarifa ya Fedha kwa kipindi cha miaka mitatu kinachoishia tarehe 31 Desemba 2023


| Mambo ya Muhimu ya Kifedha | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|
| | Shilingi '000 | Shilingi '000 | Shilingi '000 |
| Mapato ya Riba Halisi | 16,153,371 | 15,227,027 | 12,749,506 |
| Gharama za Uendeshaji | (18,724,544) | (20,667,027) | (20,711,618) |
| Mapato ya Uendeshaji | 16,539,701 | 21,634,375 | 16,117,665 |
| Jumla ya faida kabla ya Kodi | (2,184,843) | 967,348 | (4,593,953) |
| Jumla ya faida baada ya Kodi | (1,644,060) | 747,703 | (3,618,232) |
| Jumla ya Mali | 192,453,680 | 211,904,075 | 230,982,152 |
| Mikopo Halisi kwa Wateja | 114,715,813 | 120,847,669 | 120,403,894 |
| Jumla ya Amana | 125,291,419 | 141,941,494 | 140,053,421 |
| **Fedha za Wanahisa** | **27,579,007** | **28,469,252** | **24,708,478** |


### 3.8. Uwiano wa Meoneo Muhimu ya kiutendaji


| Uwiano Muhimu (%) | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|
| Mapato kwa kila hisa | Shilingi (16.8) | Shilingi 7.7 | Shilingi (37.1) |
| Thamani Halisi kwa Kila Hisa | Shilingi 282.4 | Shilingi 291.6 | Shilingi 253.3 |
| ROA (%) | (0.9%) | 0.4% | (2.0%) |
| ROE (%) | (6.0%) | 3% | (15%) |
| Uwiano wa mikopo chechefu | 11.1% | 12.2% | 6.0% |
| Uwiano Mtaji Mkuu | 14.0% | 14.4% | 12.0% |
| Uwiano wa mtaji wa Jumla | 0.4% | 0.5% | 0.4% |

### 3.9. MUHTASARI WA KIFEDHA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2023



### 3.10. Muhtasari wa Makadirio ya Fedha

- Inatarajiwa kuwa mali itaongezeka kwa asilimia 19.7 kutoka Shilingi bilioni 231.0 mwaka 2023 hadi Shilingi bilioni 276.4 kufikia mwisho wa 2024, na kwa asilimia 17.2 hadi Shilingi bilioni 323.9 mwaka 2025, na kwa asilimia 21.3 kutoka Shilingi bilioni 323.9 hadi Shilingi bilioni 392.97 kufikia Desemba 2026.
- Fedha za wanahisa zinatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 39.7 kutoka Shilingi bilioni 24.7 mwaka 2023 hadi Shilingi bilioni 34.5 kufikia mwisho wa 2024, na kwa asilimia 8.9 hadi Shilingi bilioni 37.6 kufikia Desemba 2025, na kwa asilimia 14.9 kutoka Shilingi bilioni 37.6 mwaka 2025 hadi Shilingi bilioni 43.2 kufikia Desemba 2026.
- Faida baada ya kodi inatarajiwa kuongezeka kutoka hasara ya Shilingi bilioni (3.6) mwaka 2023 hadi Shilingi milioni 551 kufikia mwisho wa Desemba 2024. Na kuongezeka mpaka kufikia shilingi bilioni 15.3 mwaka 2028.

### 3.11. Mfumo wa Uendeshaji wa DCB

DCB ni benki  inayokidhi mahitaji mbalimbali ya kibenki ya watu binafsi, biashara ndogo hadi za kati, na wateja wakubwa wa mashirika. Benki imegawanya huduma kwa wateja wake katika huduma za wateja wa reja reja, vikundi, wafanyabiashara na makampuni ili kutoa suluhisho maalum zinazokidhi mahitaji ya kipekee ya wateja.

### 3.12. Orodha ya Wanahisa Wakuu Hadi kufikia Juni 2024

| Wanahisa Wakuu | Idadi ya Hisa | Uwiano wa Umiliki |
|---|---|---|
| Umoja Unit trust Scheme | 14,091,297 | 14.32% |
| Dar es Salaam City Council | 10,228,320 | 10.48% |
| Ilala Municipal Council | 7,866,859 | 8.06% |
| UTT-Asset Management & Investor’s Service Plc (UTT-Amis) | 7,028,838 | 7.20% |
| National Health Insurance Fund | 6,000,000 | 6.14% |
| Kinondoni Municipal Council | 5,625,019 | 5.76% |
| Temeke Municipal Council | 3,422,252 | 3.50% |
| Ubungo Municipal Council | 2,877,367 | 2.95% |
| Kigamboni Municipal Council | 2,281,502 | 2.34% |
| Regular Income Unit Trust Scheme | 1,588,497 | 1.63% |
| Children’s Career Plan Unit Trust Scheme | 402,847 | 0.41% |
| UTT-Project & Infrastructure Development Plc | 100,000 | 0.10% |
| Wanahisa wengine 7,196 | 36,134,115 | 37.00% |
| **JUMLA** | **97,646,913** | **100.00** |

### 3.13. Bodi ya Wakurugenzi

| | Jina | Cheo | Uraia |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Zawadia J. Nanyaro | Mwenyekiti | Mtanzania |
| 2. | Bw. Alexander M. Sanga | Makamu Mwenyekiti | Mtanzania |
| 3. | Bi. Pamela F. Nchimbi | Mjumbe | Mtanzania |
| 4. | Dkt. Amina A. Baamary | Mjumbe | Mtanzania |
| 5. | Bi. Cliff N. Maregeli | Mjumbe | Mtanzania |
| 6. | Bw. David M. Shambwe | Mjumbe | Mtanzania |
| 7. | Bi. Hanifa S. Hamza | Mjumbe | Mtanzania |
| 8. | Prof. Tadeo A. Satta | Mjumbe | Mtanzania |
| 9. | Bw. Sabasaba K. Moshingi | Mjumbe | Mtanzania |

### 3.14. Timu ya Uongozi

| | Jina | Cheo | Uraia |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Sabasaba K. Moshingi | Mkurugenzi Mtendaji | Mtanzania |
| 2. | Bi. Regina M. Mduma | Mkurugenzi wa Sheria na Katibu wa Kampuni | Mtanzania |
| 3. | Bw. Siriaki S. Kirki | Kaimu Mkurugenzi wa Fedha | Mtanzania |
| 4. | Bw. Leonard E. Katamba | Mkurugenzi wa Teknolojia na Operesheni | Mtanzania |
| 5. | Bw. Ramadhan B. Mganga | Mkurugenzi wa Idara ya Wateja wakubwa na reja reja | Mtanzania |
| 6. | Bw. Emmanuel Y. Mushi | Kaimu Mkurugenzi wa Viashiria vya Hatari | Mtanzania |
| 7. | Bi. Msingo O. Mkanzabi | Mkurugenzi wa Rasilimali Watu | Mtanzania |
| 8. | Bw. Deogratius Thadei | Mkurugenzi wa Viashiria vya Hatari ya Mikopo | Mtanzania |
| 9. | Bw. Emmanuel O. Barenga | Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani | Mtanzania |

# 4. UTAWALA WA KAMPUNI TOAJI

## 4.1 Wajibu wa Bodi

Jukumu la msingi la Bodi ni kulinda na kuongeza thamani ya wanahisa wa muda mrefu, huku ikizingatia maslahi ya wadau wengine. Bodi inawajibika katika usimamizo wote wa wa kampuni ikiwemo kuandaa mwelekeo wake wa kimkakati, kuweka sera kwa maeneo yote ya shughuli za kampuni, kuidhinisha na kufuatilia mipango ya biashara na bajeti, kupanga mishahara, kuajiri, kusitisha ajira na kuweka sera zinazohakikisha uendelevu wa kiutendaji; kuanzisha na kusimamia na kufanikisha malengo na kuhakikisha uadilifu wa usimamizi wa hatari, huku ikizinagatia sharia na miongozo. Bodi pia ina jukumu la kuidhinisha na kufuatilia taarifa za kifedha na nyingine kwa wanahisa.

Mwaka 2023, Bodi ilikutana mara kumi na nane (18), ambapo vikao vine (4) vilikuwa vya kawaida na kumi na vinne (14) vingine vikao maalum. Bodi imekasimu utendaji wa shughuli za kila siku za kampuni kwa Mtendaji Mkuu ambaye husaidiwa na timu ya uongozi. Kamati ya uongozi hualikwa kuhudhuria vikao vya bodi na kuwezesha usimamizi wa ufanisi wa shughuli za kampuni. Mikutano ya ziada ya kawaida hujumuisha majadiliano na kuidhinisha mpango wa kila mwaka na bajeti, na kupitisha akaunti zilizokaguliwa kwa mwaka husika.

## 4.2 Muundo wa Bodi

Bodi inaundwa na wakurugenzi tisa (9) ikiwemo Mkurugenzi Mtendaji huku nane (8) wao sio watendaji, akijimuishwa na Mwenyekiti wa bodi.

## 4.3 Bodi na kamati ya Uongozi

Kazi ya kamati za Bodi ni kuisaidia Bodi katika kutekeleza majukumu yake, katika maeneo muhimu. Bodi inazo kamati tatu (3); Kamati ya Bodi ya Ukaguzi, Hatari na Uzingatiaji, Kamati ya Bodi ya Utawala na Rasilimali Watu, Kamati ya Bodi ya Mikopo.

### 4.3.1 Kamati ya Bodi ya Ukaguzina Viashiria vya Hatari na ji

Kamati ya Bodi ya Ukugaguzi, Hatari na Uzingatiaji inajumuishwa na wajumbe watatu (3). Kamati hufanya mikutano minne (4) ya kawaida na angalau mikutano miwili (2) ya dharura kwa mwaka ili kujadili ripoti za utendaji za robo mwaka, taarifa za kifedha za mwaka, na mapitio ya sera za mwaka.

Wajumbe wa Kamti ya Bodi ya Ukaguzi, Hatari na Uzingatiaji ni;

| Jina | Cheo |
|---|---|
| Prof. Tadeo A. Satta | Mwenyekiti |
| Bi. Pamela F. Nchimbi | Mjumbe |
| Bw. Cliff N. Maregeli | Mjumbe |

### 4.3.2 Kamati ya Bodi ya Utawala na Rasilimali Watu

Kamati ya Bodi ya Utawala na Rasilimali Watu inajumuishwa na wajumbe wanne (4). Kamati hufanya mikutano minne (4) ya kawaida na angalau mkutano moja (1) wa dharura kwa mwaka.

Wajumbe wa Kamati ya Utawala na Rasilimali Watu uni;

| Jina | Cheo |
|---|---|
| Bw. Alexander Sanga | Mwenyekiti |
| Bw. David Shambwe | Mjumbe |
| Bi. Hanifa Hamza | Mjumbe |
| Dkt. Amina Baamary | Mjumbe |

#### 4.3.3 Kamati ya Bodi ya Mikopo

Kamati ya Bodi ya Mikopo inajumuishwa na wajumbe wanne (4). Kamti hufanya mikutano minne (4) ya kawaida kwa mwaka.

Wajumbe wa Kamati ya Mikopo ni;

| Jina | Cheo |
|---|---|
| Bw. David M. Shambwe | Mwenyekiti |
| Bw. Alexander M. Sanga | Mjumbe |
| Bi. Hanifa S. Hamza | Mjumbe |
| Dkt. Amina Baamary | Mjumbe |

### 4.4 Hisa za Wakurugenzi

Mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2023, wakurugenzi wa DCB Commercial Bank Plc walikua na hisa za moja kwa moja na ziso moja kwa moja zinazotokana na hisa kama ilivyoonyeshwa hapa chini.

| Mkurugenzi | 2023 | 2022 |
|---|---|---|
| Bi. Zawadia J. Nanyaro | 105,240 | 21,832 |
| Bi. Pamela F. Nchimbi | 466,717 | 185,020 |
| Bw. Cliff N. Maregeli | 79,270 | 50,934 |
| Bw. David M. Shambwe | 47,399 | - |
| Bw. Alexander M. Sanga | 21,000 | - |
| Dkt. Amina A. Baamary | 9,760 | - |
| Bw. Sabasaba K. Moshingi | 67,046 | - |
| **Jumla** | **719,626** | **614,877** |

### 4.5 Wasifu wa Bodi ya Wakurugenzi

Wakurugenzi wa Kampuni huteuliwa na wanahisa kwa utaratibu kama ulivyoainishwa kwenye Hati za Kuanzishwa kwa kampuni. Ufuatao ni wasifu kwa ufupi, wa wakurugenzi wa kampuni mpaka wakati wa kuchapsihwa kwa dokezo hili:

| SN | JINA | CHEO | URAIA | SIFA NA UZOEFU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Bi. Zawadia Nanyaro**<br>(Miaka 52)<br> | Mwenyekiti asiye Mtendaji | Mtanzania | Bi. Zawadia Nanyaro ni mtaalamu mahiri na mwenye uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa ndani na wa nje, uhasibu, na utawala bora. Kwa sasa, anahudumu kama Mkurugenzi Mtendaji wa Lilac Lines Tanzania, kampuni inayojihusisha na ushauri wa ukaguzi na kodi.<br>Uzoefu wake wa awali unajumuisha nafasi katika ngazi tofauti kwenye makampuni na mashirika mbalimbali kama vile; PriceWaterhouseCoopers (PWC), Tanzania Breweries (TBL), na Mamlaka ya Ukanda wa Usindikaji Bidhaa za Nje (EPZA).<br>Ana Shahada ya Uzamili katika Utawala wa Biashara katika Fedha (MBA) na Shahada ya Biashara katika Uhasibu, zote kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ana CPA (T) ya Uhasibu wa Umma (CPA-PP), cheti cha Certified Information System Auditor (CISA), na ni Mkurugenzi aliyethibitishwa kutoka Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | **Bw. Alexander Sanga** (Miaka 46)  | Makamu Mwenyekiti asiye Mtendaji | Mtanzania | Bw. Alexander Sanga ni mtaalamu mwenye uzoefu katika teknolojia, mifumo ya taarifa, IT, na usalama wa taarifa za kidigitali. Kwa sasa, anahudumu kama Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).<br>Ana Shahada ya Uzamili ya Biashara (MBA), Certified Information Systems Audit (CISA), Certified Information Manager (CISM), Agile Expert Certified Credential (AEC), Scrum Master Certified Credential (SMC), Certified and Information System Control (CRISC), Certified in Governance of Enterprise IT (CGEIT). |
| 3. | **Bi. Pamela Nchimbi** (Miaka 43)  | Mjumbe Asiye Mtendaji | Mtanzania | Bi. Pamela Nchimbi ni mtaalamu mwenye uzoefu katika usimamizi wa uwekezaji, masoko ya mitaji, dhamana, na usimamizi wa fedha. Kwa sasa, anahudumu kama mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Uwekezaji katika UTT Asset Management and Investor Services.<br>Awali, alihudumu kama mtunza hazina katika Commercial Bank of Africa.<br>Ana Shahada ya Uzamili ya Biashara (MBA), Shahada ya Biashara (Corporate Finance), ACI dealing certificate, Fundamental Securities Certificate, Asset & Liabilities Management Certificate and Authorized dealer's Representative. Pia ni mchambuzi wa kiwango cha juu wa masuala ya kifedha (CFA). |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4. | **Bw. David Misonge Shambwe**<br>(Miaka 51)<br> | Mjumbe Asiye Mtendaji | Mtanzania | Bw. David Shambwe ni kiongozi mwenye mafanikio na matokeo chanya, akiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika kuongoza mashirika yanayokua kwa kasi.<br>Kazi yake ilianza Kibo Breweries (Diageo Group), Mkurugenzi wa Benki ya Wateja wa Rejareja katika Commercial Bank of Africa (CBA), Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara na Hazina katika Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), na Mkurugenzi Mtendaji wa Forest Development Trust. Kwa sasa anahudumu kama mshauri na Mkurugenzi Asiye Mtendaji wa Puma Energy, Bodi ya Nafaka na Mazao Mengine (CPB), DCB Commercial Bank. Majukumu yake mengine ya awali yanajumuisha kuwa mjumbe wa timu iliyounda sheria za Mikopo ya Rehani mwaka 2008/2009, mchango na muwasilishaji wa mada juu ya uwezo wa sekta ya nyumba na mikopo nchini Tanzania katika Mkutano wa Taasisi za Kifedha (COFI), Arusha 2008 uliandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania, na kuwa mjumbe wa Timu ya Kitaifa ya Ufundi kwa ajili ya Mageuzi ya Sekta ya Kifedha ya Kizazi cha Pili.<br>Ana Shahada ya Biashara katika Masoko kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Cheti cha ACI cha shughuli za masoko ya fedha (ACI-Financial Markets Associations, Oktoba-2005). |
| 5. | **Bw. Cliff Maregeli**<br>(Miaka 44)<br> | Mjumbe Asiye Mtendaji | Mtanzania | Bw. Cliff Maregeli ni mtaalamu mahiri na mwenye uzoefu mkubwa katika teknolojia ya mawasiliano, mifumo ya IT, na usalama wa taarifa za kidijitali. Kwa sasa, anahudumu kama Mkurugenzi wa ICT katika TANESCO, ambapo ameonyesha uongozi na utaalamu wa hali ya juu katika kusimamia mifumo changamano ya IT na kuhakikisha usalama wa taarifa za kidijitali.<br>Ana Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Uhandisi wa Kompyuta kutoka Chuo Kikuu cha TU Delft nchini Uholanzi, pamoja na Shahada ya Sayansi ya Uhandisi wa Kompyuta na Teknolojia ya Habari kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, ni mtaalamu aliyeidhinishwa wa usimamizi wa miradi (PMP) kutoka Taasisi ya Usimamizi wa Miradi (PMI). |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6. | **Dkt. Amina Baamary** (Miaka 48)  | Mjumbe Asiye Mtendaji | Mtanzania | Dkt. Amina Baamary ni mtaalamu mahiri na mwenye uzoefu mkubwa katika biashara, hasa katika mikopo kwa wajasiriamali na vikundi vya kujikimu. Anaelekeza juhudi zake katika Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi Vidogo na Maendeleo ya Biashara Ndogo na za Kati. Kwa sasa, anahudumu kama Mhadhiri katika Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS).<br><br>Dkt. Baamary ana Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Usimamizi wa Biashara akibobea katika Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi Vidogo na Maendeleo ya Wajasiriamali kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam/Chuo Kikuu cha Copenhagen. Pia ana Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara (MBA) katika Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shahada ya Biashara akibobea katika fedha za kampuni kutoka chuo hicho, na Stashahada ya Uhasibu kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara. |
| 7. | **Prof. (Emeritus) Tadeo Andrew Satta** (Miaka 63)  | Mjumbe Asiye Mtendaji | Mtanzania | Profesa Satta amefanya kazi za ushauri kwa wizara mbalimbali za serikali, taasisi za kifedha na kibenki, na mashirika ya ndani na ya kimataifa. Kwa sasa, ni Mkurugenzi wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Benki Kuu ya Tanzania.<br>Alianzisha Kituo cha Mafunzo ya Juu katika Utawala Bora, Ujasiriamali na Fedha (CASCEF) mwaka 2006 na alikuwa Mkurugenzi Mwanzilishi hadi Oktoba 2010.<br>Ana Shahada ya Uzamivu (Ph.D.) katika Fedha za Maendeleo kutoka Chuo Kikuu cha Manchester, Uingereza, ambapo kazi yake ya Ph.D. ilihusu Financing Micro and Small-scale Enterprises nchini Tanzania. Pia ana Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Fedha (MBA) kwa Sifa ya Juu kutoka Chuo Kikuu cha Hull, Uingereza. Aidha, ana Stashahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Fedha na Stashahada ya Juu ya Kibenki kutoka Institute of Finance Management. Utafiti na maslahi yake ya ushauri yanajikita kwenye Fedha na Maendeleo; Teknolojia za Kidijitali na Huduma za Fedha; Fedha za Biashara za Kimataifa; Usimamizi wa Hatari na Mwitikio wa Dharura; na Utawala bora na Uongozi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | **Bi. Hanifa Hamza** (Miaka 41)  | Mjumbe Asiye Mtendaji | Mtanzania | Bi. Hanifa Hamza ni mtaalamu mahiri na mwenye uzoefu katika biashara, utawala, na uongozi. Kwa sasa, anahudumu kama Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni.<br>Alijiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Biashara ya DCB Plc mwezi Mei 2022. Anawakilisha Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwenye Bodi ya Wakurugenzi ambapo ameonyesha uongozi na ustadi wa kipekee katika usimamizi.<br>Ana Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara za Kimataifa, Shahada ya Usimamizi wa Biashara, Stashahada ya Uuzaji, na Cheti cha Ujuzi wa Bima. |
| 9. | **Bw. Sabasaba Moshingi** (Miaka 54)  | Mjumbe Mtendaji (Mkurugenzi Mtendaji) | Mtanzania | Bw. Sabasaba aliteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi ya DCB Commercial Bank PLC kuwa Mkurugenzi Mtendaji mwezi Novemba 2023. Kabla ya kujiunga na DCB, Bw. Moshingi alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Commercial Bank (TCB) kwa miaka 12. Wakati wa wake kama Mkurugenzi Mtendaji, TCB ilibadilika kutoka benki ndogo yenye mali ya jumla ya Shilingi bilioni 121 hadi Shilingi trilioni 1.4, na kuiweka kuwa miongoni mwa benki kubwa zaidi nchini Tanzania.<br>Kabla ya kujiunga na TCB, Bw. Moshingi alikuwa Mkuu wa Kanda wa Hatari za Uendeshaji wa Huduma za Wateja na Usimamizi wa Mauzo katika Benki ya Standard Chartered kuanzia mwaka 2007 katika eneo la Ghuba ya Kaskazini, Levant, na Oman (kanda iliyojumuisha nchi tano ambazo ni Jordan, Lebanon, Qatar, Oman, na Bahrain) - akiwa na makao makuu katika Ufalme wa Bahrain.<br>Pia ni Mjumbe wa Bodi na Mwenyekiti wa Tigopesa Tanzania, Mjumbe wa Bodi wa Taasisi ya Benki za Akiba na Rejareja Duniani (WSBI yenye makao makuu mjini Brussels, Ubelgiji), Mjumbe wa Baraza la Utawala na Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu ya Taasisi ya Mabenki Tanzania, Mjumbe wa Bodi na Mwenyekiti wa UmojaSwitch Company Limited, Mjumbe wa Bodi na Mwenyekiti wa UBX Tanzania Limited, Mjumbe wa Bodi wa TMRC na ni Mwanachama wa Eisenhower Fellowship yenye makao makuu Marekani. Bw. Moshingi ni mwanabenki mwenye sifa na ana Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara (Fedha) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. |

### 4.6 Timu ya Uongozi

Kwa sasa timu ya Uongozi inawajumuisha Mkurgenzi Mtendaji, Mkurugenzi wa Sheria na Katibu wa Kampuni, Mkurugenzi wa Fedha, Mkurugenzi wa Teknolojia na Operesheni, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Mkurugenzi wa Benki ya Rejareja na Biashara, Mkurugenzi wa Hatari ya Mikopo, Mkurugenzi wa Hatari na Uzingatiaji, na Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani

| SN | Jina, Cheo na Uraia | Taaluma na Uzoefu wa Kazi |
|---|---|---|
| 1. | **Bw. Sabasaba Moshingi**<br>Mkurugenzi Mtendaji<br>Mtanzania (Miaka 54)<br> | Tazama wasifu wa Wakurugenzi hapo juu. |
| 2. | **Bi. Regina Mduma**<br>Mkurugenzi wa Shera na Katibu wa Kampuni<br>Mtanzania (Miaka 44)<br> | Regina Mduma ni mtaalamu wa sheria mwenye uzoefu wa miaka kumi na tisa (19) katika taaluma ya sheria. Ni mtaalamu wa utawala bora wa mashirika, sheria za benki na fedha, sheria za biashara za kimataifa, sheria za bima, mikataba ya kimataifa, na usuluhishi. Ana Shahada ya Uzamili ya Sheria (LLM) katika Sheria za Uagizaji na Uuzaji wa Bidhaa (Sheria za Biashara ya Kimataifa) kutoka Chuo Kikuu cha North-West, Kampasi ya Potchefstroom nchini Afrika Kusini, na Shahada ya Sheria (LLB) kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Lesotho. Regina aliruhusiwa kufanya kazi kama Wakili na Mwanasheria katika nchi tatu tofauti (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ufalme wa Lesotho, na Jamhuri ya Botswana), hali iliyomuwezesha kupata ujuzi katika mifumo ya sheria ya Kiingereza na Sheria ya Kirumi ya Kiholanzi.<br>Mbali na sifa zake nzuri, Bi. Mduma ana vyeti vya bima ya muda mfupi (Bima ya Jumla) na ya muda mrefu (Bima ya Maisha) kutoka Taasisi ya Bima ya Afrika Kusini (IISA) na Chuo cha Uhasibu cha Botswana, mtawalia. Pia ameidhinishwa kama Katibu wa Kampuni na Mkurugenzi na Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania (IoDT). Regina ni mwanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika na Chama cha Wanasheria Afrika Mashariki. Pia ni mwanachama asiyefanya mazoezi wa Chama cha Wanasheria Lesotho na Chama cha Wanasheria Botswana. |

3. **Bw. Siriaki Surumbu**

Kaimu Mkurugenzi wa Fedha

Mtanzania (Miaka 37)



Bw. Siriaki ni mwanabenki mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 13 katika sekta ya benki na kwa sasa anahudumu kama Kaimu Mkurugenzi wa Fedha katika benki ya DCB Commercial Bank PLC. Katika kazi yake katika DCB, ameshika nafasi muhimu kama Meneja wa Fedha na Meneja wa Utendaji wa Biashara na Uchambuzi. Utaalamu wake katika uandaaji wa ripoti za kifedha, mikakati ya biashara, na usimamizi wa mizania umechangia sana katika ufanisi wa kiutendaji wa benki na mipango ya kimkakati.

Siriaki ana Shahada ya Biashara (Uhasibu) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni Mhasibu aliyeidhinishwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

4. **Bi. Msingo Mkanzabi**

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu

Mtanzania (Miaka 44)



Msingo Mkanzabi ni Mkurugenzi wa Rasilimali Watu katika DCB. Ana jukumu la kuandaa na kutekeleza mkakati wa rasilimali watu na ununuzi ili kuunga mkono mipango ya jumla ya benki na mipango ya kimkakati. Hasa, anasimamia mipango ya warithi, usimamizi wa vipaji, usimamizi wa mabadiliko, usimamizi wa shirika na utendaji, mafunzo na maendeleo, malipo, usimamizi wa wauzaji, vifaa, na usimamizi wa ofisi.

Msingo ana Shahada ya Heshima ya Saikolojia ya Viwanda na Shirika kutoka Chuo Kikuu cha Afrika Kusini na Shahada ya Sayansi ya Jamii katika Masomo ya Viwanda, Shirika na Kazi kutoka Chuo Kikuu cha Cape Town. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 17 katika kutoa huduma za ushauri wa rasilimali watu katika sekta mbalimbali Afrika Mashariki. Alifanya kazi kama Meneja wa Deloitte Consulting Limited kabla ya kujiunga na DCB.

5. **Bw. Emmanuel Yakobo Mushi**

Kaimu Mkurugenzi wa Hatari na Uzingatiaji

Mtanzania (Miaka 41)



Emmanuel ni mtaalam wa benki mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 14 na kwa sasa anahudumu kama Kaimu Mkurugenzi wa Hatari na Uzingatiaji. Katika nafasi hii, ana jukumu la kuandaa na kutekeleza mkakati wa jumla wa hatari wa benki pamoja na kusimamia uzingatiaji, mikopo, operesheni, na hatari za soko ili kuhakikisha inalingana na malengo ya biashara ya benki.

Kabla ya nafasi hii, Emmanuel alishika nafasi muhimu ndani ya DCB, ikiwa ni pamoja na Afisa Mkuu wa Hatari na Uzingatiaji na Afisa wa Fedha. Pia amefanya kazi kama Afisa wa Fedha katika Benki ya Biashara ya Kimataifa (T) LTD na alianza kazi yake kama Mwanafunzi wa Afisa wa Fedha katika Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) Limited.

Emmanuel ana Stashahada ya Juu ya Uhasibu kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania na Cheti cha Kitaaluma katika Usimamizi wa Mtandao kutoka Kituo cha Kompyuta cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa sasa anasomea Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Fedha na Uwekezaji katika Taasisi ya Usimamizi wa Fedha.

6. **Bw. Deogratius Thadei**
Mkurugenzi wa Hatari ya Mikopo
Mtanzania (Miaka 37)



Deogratius Thadei ni mhasibu mwenye sifa na uzoefu wa zaidi ya miaka 9 katika ukaguzi, uhasibu, na fedha. Amefanya kazi na Deloitte & Touche na Benki ya First National Tanzania. Deogratius ana msingi imara katika fedha, ikijumuisha upangaji wa bajeti, utabiri, ununuzi, usimamizi wa mtiririko wa fedha, na maarifa kuhusu masuala ya kodi ya Tanzania. Ni kiongozi bora mwenye rekodi ya kuboresha usimamizi wa kifedha na uandaaji wa ripoti, kurahisisha shughuli na michakato, na kuboresha udhibiti wa ndani.

Deogratius ana cheti cha Mhasibu Aliyeidhinishwa (ACPA-T) kutoka Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania na Shahada ya Biashara katika Uhasibu na Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe. Yeye ni mwanachama wa Chama cha Wahasibu na Wakaguzi wa Kitaalamu (ACCA - UK) na Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Tanzania.

Rekodi yake ya ajira inajumuisha kazi kama Meneja wa Ukaguzi wa Ndani katika Benki ya First National Tanzania na nafasi mbalimbali katika Deloitte & Touche Tanzania, ikiwa ni pamoja na Msaidizi wa Ukaguzi, Msaidizi Mwandamizi wa Ukaguzi, na Mwandamizi wa Ukaguzi. Deogratius ana uzoefu wa kusimamia timu za ukaguzi, kutathmini udhibiti wa ndani, kukagua taarifa za kifedha, na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na kanuni.

7. **Bw. Ramadhan Mganga**
Mkurugenzi wa Benki ya Rejareja
Mtanzania (Miaka 45)



Bw. Ramadhan Mganga alijiunga na DCB Commercial Bank kama Mkurugenzi wa Benki ya Wateja binafsi mwezi Julai 2024, akihusika na kuendesha shughuli za biashara ya rejareja na mkakati wa benki wa kufikia ukuaji endelevu wa biashara.

Kabla ya kujiunga na DCB, alifanya kazi na Tanzania Commercial Bank (TCB) kama Meneja Mkuu wa Fedha za Vikundi na na Tanzania Postal Bank kama Meneja Mwandamizi wa Rejareja.

Anashahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara - Usimamizi wa Mashirika kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, na Shahada ya Sayansi ya Misitu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA). Pia ana cheti cha Fedha za Vikundi (Microfinance) kilichotolewa na Kituo cha Global Development Learning, Tokyo, Japan, na ni mtaalam anayekubalika na mkufunzi aliyethibitishwa kikamilifu katika masuala ya Fedha za Vikundi.

8. **Bw. Leonard Emmanuel Katamba**

Mkurugenzi wa Teknolojia na Operesheni

Mtanzania (Miaka 42)



Bw. Katamba alijiunga na DCB mwaka 2024 kama Mkurugenzi wa Uendeshaji na Teknolojia, akiwa na uzoefu wa miaka 16 wa maendeleo, na sifa za kuandaa na kutekeleza mikakati ya jumla inayounganisha uvumbuzi wa teknolojia na ufanisi wa kiutendaji ili kuleta mabadiliko ya kidijitali.

Kabla ya kujiunga na DCB, alifanya kazi na Tanzania Commercial Bank (TCB) na CBA Bank (sasa NCBA), ambako alijipatia sifa nzuri ya uongozi wa kimuundo na ushirikiano wa kimkakati katika kuendesha uvumbuzi na mabadiliko ya kidijitali katika benki.

Ana Shahada ya Sayansi ya Kompyuta kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mafunzo ya ziada katika uongozi, ushirikiano, uhamasishaji wa michakato, usimamizi wa miradi, usimamizi wa bidhaa za kidijitali, na ubora wa uendeshaji.

9. **Bw. Emmanuel O. Barenga**

Mkurugenzi was Ukaguzi wa Ndani

Mtanzania (Miaka 34)



Emmanuel Barenga ni mtaalamu mwenye ujuzi anayeweza kubadilika na mafanikio yaliyothibitishwa katika kuongoza ukaguzi wa ndani na kazi za ushauri, akiwa na rekodi nzuri ya kuboresha ubora wa kiutendaji. Ana uwezo wa kuongoza timu za kifunctional mbalimbali, kufundisha vipaji vinavyochipukia, na kukuza utamaduni wa maboresho endelevu na uvumbuzi.

Kabla ya kujiunga na DCB Commercial Bank, alifanya kazi na Deloitte East Africa katika kitengo cha Huduma za Ushauri wa Hatari na Golden Land Group (kwa sasa China-Dasheng Commercial Bank) kama mwanafunzi wa mafunzo ya uongozi wa wahitimu akiwa Nanjing, China.

Ana Shahada ya Uzamili katika Fedha na Uwekezaji kutoka Taasisi ya Usimamizi wa Fedha, Shahada ya Kwanza katika Sayansi ya Actuarial, Stashahada ya Uzamili ya Uhisabati wa Kisayansi (Artificial Intelligence na Machine Learning) zote kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni Mhasibu aliyesajiliwa (CPA-T), Mkaguzi wa Mifumo ya Habari aliyethibitishwa (CISA), mwenye Cheti cha Udhibiti wa Hatari na Mifumo ya Habari (CRISC), na Meneja wa Usalama wa Habari aliyethibitishwa kutoka ISACA, na pia ana Cheti cha Uchambuzi wa Mikopo ya Kibenki kilichotolewa na Taasisi ya Fedha ya Biashara (Corporate Finance Institute).

## 5. VIASHIRIA VYA HATARI

Uwekezaji wowote una vihatarishi vyake. Ni muhimu kwa wawekezaji kujua hatari hizo, hasa wanahisa wa DCB Commercial Bank PLC ambao watashiriki na kunufaika katika suala hili la Hisa za Upendeleo. Hatari zinaweza kuathiri shughuli za Kampuni na kusababisha hasara, ikiwa hazitatambuliwa kwa uangalifu, kufuatiliwa, kudhibitiwa na kupunguzwa. Ieleweke kwamba, bei za hisa na dhamana nyinginezo kwenye soko la hisa zinaweza kupanda au kushuka na hakuna uhakika kwamba bei nzuri za wakati uliopita zinaweza kujirudia tena au la. Wawekezaji wanapaswa kuzingatia kwa makini hatari zilizofafanuliwa hapa chini, pamoja na maelezo mengine yaliyomo katika Dokezo hili, kabla ya kufanya uamuzi wowote wa uwekezaji. Hatari na mambo ya kutokuwepo kwa uhakika ambayo kwa sasa hayajulikani au yanayochukuliwa kuwa madogo yanaweza pia kuathiri utendaji wa shughuli za benki na matokeo yake ya kifedha.

Bodi ya Wakurugenzi ina wajibu wa jumla wa kuanzisha na kusimamia mfumo wa udhibiti wa vihatarishi. Kama sehemu ya muundo wake wa utawala, Bodi ya Wakurugenzi imeunda Kamati ya Bodi ya Ukaguzi, Hatari na Uzingatiaji ili kuisaidia katika kutambua, kupima, kudhibiti (kuweka mbinu za kudhibiti vihatarishi) na ufuatiliaji wa vihatarishi. Bodi ya Wakurugenzi itakuwa ndiyo mwajaibikaji wa mwisho katika kuhakikisha udhibiti wa vihatarishi na usimamizi wa shughuli za ndani.

### 5.1 Vihatarishi Vinavyohusiana na Mtoaji wa Hisa

Kutokana na aina ya biashara na shughuli zake, benki inakabiliwa na hatari zifuatazo kutokana na shughuli zake za kibiashara na matumizi ya vyombo vya kifedha. Mfumo wa usimamizi wa hatari wa benki umeundwa ili kubaini, kutathmini, kupunguza, na kufuatilia hatari hizi ili kuhakikisha utulivu wa kifedha, kufuata matakwa ya kisheria, na kulinda thamani ya wanahisa. Hatari kuu zinazoikabili benki zimeelezwa hapa chini:

#### 5.1.1 Vihatarishi fedha

Hatari za kifedha zinajumuisha hatari za ukwasi na mkopo. Usimamizi wa hatari za benki kwa ujumla unahusisha kubaini mapema hatari hizi, kupunguza athari zake, na kuzifuatilia kwa kuendelea ili kuhakikisha benki inaweza kutimiza majukumu yake na kufikia malengo yake ya kimkakati. Hatari kuu za kifedha zimeelezwa hapa chini:

- **Vihatarishi vya Ukwasi**

Hatari ya ukwasi ni hatari kwamba benki haitakuwa na fedha za kutosha kutimiza majukumu yake ya kifedha. Kukosa kudumisha ukwasi wa kutosha kunaweza kudhoofisha uwezo wa benki kuendesha shughuli za kila siku, kulipa madeni, na kutimiza mahitaji ya ukwasi ya kisheria, na hivyo kusababisha kuvuruga shughuli na kupoteza imani ya soko.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Benki inasimamia hatari ya ukwasi kwa kupitia mara kwa mara nafasi yake ya ukwasi, ahadi zake za baadaye, na mikopo iliyopo.

Aidha, benki hufanya makadirio ya mtiririko wa fedha kwa kutumia utabiri, kufanya majaribio ya dhiki (stress tests) na uchambuzi wa hali mbaya ili kutathmini uwezo wake wa kutimiza majukumu chini ya mazingira magumu.

- **Vihatarishi vya Mikopo**

Hatari ya mkopo ni hatari ya hasara ya kifedha inayotokana na kushindwa kwa mshirika wa kibiashara kutimiza majukumu yake ya kimkataba. Hatari hii ni ya msingi katika shughuli za kukopesha za benki, portifolio za uwekezaji, na shughuli nyingine za kifedha

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Benki inatumia mfumo madhubuti wa usimamizi wa hatari ya mkopo unaojumuisha tathmini makini ya mikopo, kuweka mipaka sahihi ya mikopo, na kufuatilia kwa kuendelea uwekezaji wa mikopo na kutawanya portifolio yake ya mikopo katika sekta mbalimbali na aina za washirika wa kibiashara ili kupunguza hatari ya mkusanyiko.

#### 5.1.2 Vihatarishi vya Uendeshaji

Benki inakabiliwa na hatari za uendeshaji ambazo zinaweza kutokea kutokana na mchakato, watu, mifumo, au matukio ya nje ambayo hayatoshi au yamekosa. Hatari hii inajumuisha udanganyifu, vitisho vya usalama wa mtandao, na usumbufu wa uendeshaji.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Sera na mifumo ya usimamizi wa hatari inakaguliwa mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba udhibiti wote unabaki kuwa wa kutosha katika kupunguza hatari za uendeshaji zilizomo. Mafunzo ya mara kwa mara na programu za uhamasishaji zinafanywa ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanaelewa mfumo wa hatari za uendeshaji na wanatii sera zinazohusiana pamoja na mipango ya usimamizi wa matukio na uendelevu wa biashara.

### 5.1.3 Vihatarishi vya Uzingatiaji Sheria

Hatari hii inaweza kuifanya kampuni kukabiliwa na faini, adhabu za kisheria, malipo ya fidia, kufutwa kwa mikataba, na hatari kwa mapato au mtaji kutokana na ukiukwaji wa sheria, kanuni, sera na taratibu za ndani, au viwango vya kimaadili. Hatari hii ni muhimu hasa katika sekta ya benki, ambapo mazingira ya udhibiti ni magumu na yanabadilika mara kwa mara.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Kampuni imeweka sera zinazodhibiti ugunduzi, kuzuia, kufuatilia, na kuripoti hatari ya kufuata sheria kwa ajili ya udhibiti, kwa mifumo ya kisheria na sera za ndani ya benki. Mfumo wa usimamizi wa kufuata sheria umepangwa, ambao unajumuisha ufuatiliaji wa mara kwa mara na ukaguzi wa mabadiliko ya kisheria, programu za mafunzo kwa wafanyakazi, na ukaguzi wa mara kwa mara wa kufuata sheria na tathmini za hatari ili kubaini maeneo yanayoweza kuwa na ukosefu wa kufuata sheria na kuchukua hatua za kurekebisha haraka.

### 5.1.4 Vihatarishi vya Kimkakati

Viahatrishi vya kimkakati ni vile hatari vinavyotokana na uundwaji wa mbinu na mipango vya kimkakati, mipango ya kibiashara na utekelezaji wa mipango isiyofaa na isiyoendana na mambo ya ndani na mazingira ya nje, ambayo yanaweza kuathiri mapato, mtaji, au ustawi na uendelevu wa biashara.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Ili kuepuka vihatarishi vya kimkakati, Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Juu huunda kwa umakini mipango ya kistratejia na ya kibiashara, inayosaidia utawala bora wa kampuni, pamoja na kuweka miundombinu ya ndani inayofaa kwa utekelezaji wa mipango na mikakati.

### 5.1.5 Vihatarishi Katika Sifa

Hatari ya sifa ni uwezekano kwamba taarifa mbaya kuhusu mienendo ya biashara ya kampuni, iwe ya kweli au ya uongo, inaweza kusababisha kupoteza imani ya wateja, kushuka kwa bei ya hisa zake, au kusababisha mashtaka yenye gharama kubwa. Hatari hii inaweza kutokea kutokana na kushindwa kwa kampuni kusimamia vyema aina nyingine za hatari.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Uwajibikaji wa mwisho wa usimamizi wa hatari ya sifa upo mikononi mwa Bodi. Bodi ya Wakurugenzi inatambua wazi hatari ya sifa kama hatari inayojitegemea na inayoweza kudhibitiwa kwa usalama na uimara wa kampuni kupitia mfumo wa kina wa usimamizi wa hatari ya sifa.

## 5.2 Vihatarishi Vinavyohusiana na Masoko

Hatari ya soko ni hatari ya hasara inayotokana na mabadiliko ya bei za soko, ikijumuisha viwango vya riba, viwango vya kubadilisha fedha za kigeni, na bei za hisa. Hatari ya soko inaathiri mapato na mtaji wa benki, hasa kupitia shughuli zake za mikopo, uwekezaji, na biashara.

### 5.2.1 Hatari ya Kiwango cha Riba

Hatari ya kiwango cha riba ni hatari kwamba mabadiliko katika viwango vya riba yataathiri vibaya utendaji wa kifedha wa benki. Hatari hii inatokana na kutokulingana katika muda wa ukomavu na upangaji upya wa mali na madeni ya benki, ambayo inaweza kusababisha kupungua kwa faida halisi ya riba, mabadiliko ya thamani ya mali zinazotegemea viwango vya riba, na athari zinazowezekana kwenye mapato na mtaji.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Ili kupunguza hatari hii, kampuni inatofautisha uwekezaji wake katika dhamana mbalimbali zenye vipindi tofauti vya ukomavu ili kupunguza hatari zinazotokana na uwekezaji katika dhamana za mapato ya kudumu.

#### 5.2.2 Hatari ya Fedha za Kigeni

Hii ni hatari ya mabadiliko katika viwango vya kubadilisha fedha yataathiri vibaya utendaji wakifedha wa benki. Hatari hii inatokana na mfiduo wa benki kwa mali, madeni, na vipengele vilivyo nje ya mizania vilivyo katika sarafu za kigeni, pamoja na shughuli zake za biashara katika masoko ya kubadilisha fedha za kigeni.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Benki ina mfumo madhubuti unaojumuisha ufuatiliaji na usimamizi wa viwango vya kubadilishana fedha kila siku.

#### 5.2.3 Hatari za Kisiasa

Tanzania, kama nchi nyingi zinazoendelea, inakabiliwa na matukio ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii ambayo yanaweza kuleta hatari kwa wawekezaji. Hatari hizi ni ngumu zaidi kutabiri na kupima kuliko katika nchi zilizoendelea. Hata hivyo, mazingira ya kisiasa ya Tanzania ni salama na thabiti kwa shughuli za biashara.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Benki hufanya uchambuzi wa hatari kwa kupitia mawakala wa kibiashara wa kigeni ili kuelewa soko, mfumo wa kisiasa, na hatari mahususi za ndani.

### 5.3 Vihatarishi Vinavyohusiana na Hisa Zinazotolewa

#### 5.3.1 Mabadiliko ya Bei ya Hisa

Bei ya hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa inaweza kubadilika mara kwa mara kutokana na hali ya soko, mambo ya kiuchumi, au mabadiliko za mtazamo wa wawekezaji. Bei nzuri za wakati uliopita zinaweza kujirudia tena au la, na utendaji wa hisa wakati wa nyuma hauhakikishi faida za baadaye.

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Wanahisa wanashauriwa kushauriana na washauri wao wakitaalamu wa uwekezaji kabla ya kufanya uamuzi wa kuwekeza. Aidha, wanahisa wanahimizwa kuchukua mkakati wa uwekezaji wa muda mrefu ili kupunguza athari za mabadiliko ya bei ya muda mfupi na kunufaika na thamani ya muda mrefu inayoweza kuongezeka.

#### 5.3.2 Hatari ya Kupungua kwa Asilimia ya Umiliki wa Hisa

Wanahisa waliopo ambao hawatashiriki katika kununua hisa za upendeleo wako katika hatari ya kupunguzwa kwa asilimia ya umiliki wao wa hisa katika kampuni

**Mkakati wa Kupunguza Hatari**

Wanahisa wanahimizwa kushiriki katika utoaji hisa za upendeleo ili kuepuka kushuka kwa asilimia zao za umiliki katika benki ya DCB. kupungukiwa kwa umiliki wao.

## 6. TAARIFA ZA KISHERIA

### 6.1. Maelezo Juu ya Usajili

Benki ilisajiliwa tarehe 6 Septemba 2001ikiwa nan amba ya usajili 42904, chini ya Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 (baadaye ilifutwa na Sheria ya kampuni Na. 12 ya 2002) na imeorodheshwa kwenye soko la Hisa la Dar es Salaam. Benki ya Tanzania ilitoa leseni chini ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha Na. 5 ya 2006.

### 6.2. Ofisi za Kampuni toaji

Ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni iko DCB House, Magomeni Mwembechai, Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam, na anwani ya Posta ni S.L.P 19798, Dar es Salaam.

### 6.3. Mtaji wa Hisa Ulioidhinishwa na Kutolewa

Mtaji ulioruhusiwa wa kampuni kufikia tarehe 31 Desemba 2023 ulikuwa Shilingi 100,000,000,000.00 ukiwa umegawanywa katika hisa za kawaida 400,000,000 zenye thamani ya Shilingi 250 kila moja.

Mtaji uliotolewa na kulipwa kikamilifu wa kampuni kufika tarehe 31 Desemba 2023 ulikuwa Shilingi 24,411,725,750 ukiwa umegawanwa katika hisa za kawaida 97,646,913 zenye thamani ya Shilingi 250 kila moja. Wamiliki wa hisa za kawaida wana haki ya kupokea gawio lililotangazwa mara kwa mara.

### 6.4. Sera ya Gawio

Kutangazwa kwa gawio hutegemea mahitaji ya kisheria, pendekezo na idhini la Wakurugenzi na idhini ya Mkutano Mkuu wa Mwaka na hali ya kifedha ya Kampuni.

AUDITAX International
Head Office - Dar es Salaam: Auditax House, 3rd Floor | Coca-Cola Road
P. O. Box 77949 Dar es Salaam
M: +255 719 878490 |T: +255 22 212 692
Email: info@auditaxinternational.co.tz
Website: www.auditaxinternational

## 6. RIPOTI YA MHASIBU

24-Sep-24

**Utangulizi wa Kuripoti Taarifa ya Mhasibu**

Kwenda kwa,

Wakurugenzi,

DCB House,

Plot No. 182 Block R, Magomeni Mwembechai,

Barabara ya Morogoro,

S.L.P 19798, Dar es Salaam.

Tunawasilisha ripoti yetu ya Mhasibu kwa Mujibu wa Masharti ya Sehemu ya Tatu, Kifungu cha 13 cha Kanuni za Masoko la Mitaji na Dhamana za Tanzania na Sehemu ya IV ya Kanuni za PLC za Soko la Hisa la Dar es Salaam, za mwaka 2022, zitakazojulikana hapa chini kama "Kanuni".

Tumepitia taarifa za fedha zilizokaguliwa za DCB Commercial Bank Plc ("Kampuni") kwa vipindi vifuatavyo:

a) Mwaka ulioishia 31 Desemba 2023
b) Mwaka ulioishia 31 Desemba 2022
c) Mwaka ulioishia 31 Desemba 2021 Iliyorudiwa

**Wajibu wa Wakurugenzi**

Wakurugenzi wa DCB Commercial Bank Plc (DCB) wanawajibika kuandaa na kwa usahihi taarifa za kihistoria za fedha za DCB Commercial Bank Plc kwa miaka iliyoishia tarehe 31 Desemba 2023, 31 Desemba 2022 na zilizorudiwa za 31 Desemba 2021, na kuandaa na kuwasilisha taarifa ya fedha iliyotabiriwa kwa miaka zinazoishia 31 Desemba 2024, 2025, 2026, 2027 na 2028, na mtiririko wa fedha kwa hiyo miaka. ("Taarifa Zilizotabiriwa za Kifedha") na mawazo ambayo kwayo imetayarishwa ("Mawazo ya Wakurugenzi").

Taarifa za kisheria za kifedha kwa miaka iliyoishia tarehe 31 Desemba 2023, 31 Desemba 2022, na 31 Desemba 2021 zilikaguliwa na PricewaterhouseCoopers Limited na kupokea hati safi za ukaguzi.

**Wajibu wetu kama wahasibu wotoa taarifa**

Wajibu wetu umefafanuliwa kwa kina katika barua yetu ya makubaliano. Wajibu huu ni pamoja na kuandaa Ripoti ya Mhasibu wa Taarifa ambayo inajumuisha yafuatayo:

a) Taarifa Huru ya Mapitio ya Taarifa za Kihistoria za Fedha kwa mujibu wa ISRE 2400 (Iliyorekebishwa).

b) Taarifa ya majumuisho kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79 R.E (2002) iliyofanyiwa marekebisho na kwa kuzingatia Sheria za Tanzania na Kanuni za Dhamana za Tanzania na Sehemu ya IV ya Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam za mwaka 2016, zitakazojulikana hapa chini kama "Kanuni" na Viwango vya Kimataifa vya Huduma Zinazohusiana zinazotumika kwa mashirikiano ya ujumuishaji (ISRS) 4410 kama ilivyobainishwa katika taarifa hii.

c) Maelezo kuhusu taarifa za fedha zilizotabiriwa kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka unaomalizika tarehe 31 Desemba 2024 hadi 31 Desemba 2028, na mtiririko wa fedha wao, ikiwa ni pamoja na hitimisho la uhakikisho mdogo kuhusu uhalali wa Dhana za Wakurugenzi na maoni kuhusu Taarifa za Kifedha zinazotarajiwa kwa mujibu wa Kiwango cha Kimataifa cha Uhakikisho kinachohusiana na uchunguzi wa taarifa za kifedha zinazoweza kutokea (ISAE) 3400 Uchunguzi wa Taarifa za Kifedha zinazoweza kutokea, katika taarifa hii.

**Idhini**

Tunaidhinisha kujumuishwa kwa taarifa hii kwenye Toleo la Hisa za Upendeleo wa kampuni ya CDB Commercial Bank Plc linalotarajiwa kutoka mwezi Septemba mpaka Oktoba 2024 au baada ya hapo, katika muundo na namna toleo hilo linavyoonekana.

Mshirika wa makubaliana haya atakayewajbika na yote yaliyomo kwenye Taarifa hii ni CPA Khalfani Mwambo (ACPA 3224)

**Kwa niaba ya:**

Auditax International,

Certified Public Accountants (T)

S.L.P 77949

Dar es Salaam, Tanzania

.......................................

Imesainiwa na: CPA Khalfani Mbwambo (ACPA – 3224)

Tarehe: 24 Septemba 2024

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA ULIOSHIA 31 DECEMBER 2023, 2022, AND 2021

| | 2023 SHILINGI '000 | 2022 SHILINGI '000 | 2021 SHILINGI '000 Restated |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 27,835,426 | 28,607,305 | 27,617,664 |
| Gharama za Riba | (15,085,920) | (13,380,278) | (11,464,293) |
| **Mapato Halisi ya Riba** | **12,749,506** | **15,227,027** | **16,153,371** |
| Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,109,550) | (3,874,865) | (6,503,867) |
| **Mapato ya Riba baada ya Kupunguza Tengo katika Mikopo** | **9,639,956** | **11,352,162** | **9,649,504** |
| Ada na Kamisheni | 4,880,621 | 5,751,715 | 4,826,434 |
| Faida Zitokanazo na Miamala ya Fedha Za Kigeni | 364,191 | 386,107 | 280,258 |
| Mapato Mengine | 1,232,897 | 4,144,391 | 1,783,505 |
| **Mapato Yasiyo na Riba** | **6,477,709** | **10,282,213** | **6,890,197** |
| **Mapato ya Uendeshaji** | **16,117,665** | **21,634,375** | **16,539,701** |
| **Gharama za Uendeshaji** | | | |
| Mishahara na Mafao | (10,042,148) | (9,993,648) | (9,765,285) |
| Matumizi ya Utawala kwa ujumla | (6,817,215) | (8,052,221) | (6,435,238) |
| Matumizi ya kupungua thamani | (3,852,255) | (2,621,158) | (2,524,021) |
| **Jumla ya Gharama za Uendeshaji** | **(20,711,618)** | **(20,667,027)** | **(18,724,544)** |
| **Faida/(Hasara) Halisi Kabla ya Kodi ya Mapato** | **(4,593,953)** | **967,348** | **(2,184,843)** |
| **Tengo la Kodi ya Mapato** | 975,721 | (219,645) | 540,783 |
| **Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(3,618,232)** | **747,703** | **(1,644,060)** |
| Mapato mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | (142,542) | 142,542 | (163,681) |
| **Jumla ya mapato kamili kwa mwaka** | **(3,760,774)** | **890,245** | **(1,807,741)** |
| **(Hasara)/faida kwa kila hisa (msingi na iliyodondoshwa)** | **(37)** | **8** | **(17)** |

## TAARIFA YA MIZANIA KWA MWAKA HADI TAREHE 31 DECEMBER 2023, 2022, AND 2021

| | 2023<br>SHILINGI '000 | 2022<br>SHILINGI '000 | 2021<br>SHILINGI '000<br>Restated |
|---|---|---|---|
| **Mali** | | | |
| | | | |
| Fedha taslimu na Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 21,576,928 | 19,005,746 | 20,053,560 |
| Uwekezaji katika Amana za Serikali – FVOCI | - | 27,639,102 | - |
| Amana za Serikali – (Amortized cost) | 57,156,768 | 13,663,360 | 28,616,539 |
| Uwekezaji wa Hisa – FVOCI | 2,040,200 | 2,040,200 | 2,040,200 |
| Salio katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,271,278 | 3,963,844 | 2,286,048 |
| Mikopo Halisi Iliyopo | 120,403,894 | 120,847,669 | 114,715,813 |
| Corporation tax recoverable | 975,000 | 2,095,060 | 2,085,029 |
| Deferred income tax asset | 7,053,824 | 5,210,033 | 5,206,655 |
| Mali Nyingine | 3,001,042 | 3,230,825 | 2,187,779 |
| Haki ya matumizi ya Mali | 6,890,965 | 5,494,196 | 6,305,536 |
| Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,981,231 | 3,646,824 | 3,845,700 |
| Mali Zisizoshikika | 3,631,022 | 5,067,216 | 5,110,821 |
| **Jumla Ya Mali** | **230,982,152** | **211,904,075** | **192,453,680** |
| | | | |
| **Dhima** | | | |
| Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 47,664,218 | 23,934,235 | 24,749,752 |
| Amana za Wateja | 140,053,421 | 141,941,494 | 125,291,419 |
| Madeni | 11,213,836 | 11,900,791 | 8,426,352 |
| Dhima Nyingine | 2,862,953 | 2,774,670 | 2,860,555 |
| Dhima za mkataba za Kukodishwa | 4,479,246 | 2,883,633 | 3,546,595 |
| **Jumla ya Dhima** | **206,273,674** | **183,434,823** | **164,874,673** |
| | | | |
| **Fedha za Wanahisa** | | | |
| Mtaji wa Hisa Uliolipiwa | 24,061,904 | 24,061,904 | 24,061,904 |
| Akiba ya mtaji | 4,183,291 | 4,183,291 | 4,183,291 |
| Advance towards share capital | - | - | 0 |
| Mapato Yaliyobakizwa | (4,145,700) | (3,792,602) | (4,751,930) |
| Regulatory banking risk reserve | 130,043 | 3,395,177 | 3,606,802 |
| Fair valuation reserve | 478,940 | 621,482 | 478,940 |
| **Jumla ya Fedha za Wanahisa** | **24,708,478** | **28,469,252** | **27,579,007** |
| | | | |
| **Jumla ya Mtaji na Dhima** | **230,982,152** | **211,904,075** | **192,453,680** |

## 7. FOMU YA MAOMBI

### FOMU YA DCB COMMERCIAL BANK PLC YA KUPATA HISA ZA UPENDELEO

Nakala ya Dokezo ambayo maombi haya yameambatanishwa ilisajiliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 na Kifungu cha 131 cha Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79 (kama ilivyorekebishwa).

Fomu ya Maombi ni ya Hisa za Kawaida za DCB Commercial Bank PLC kwa namna ya kupata Hisa za Upendeleo ya kununua hisa kwa wanahisa waliopo na/Au Muidhinishaji kwa hisa za kawaida zinazotolewa kwa hisa 97,646,913 za kawaida kwa bei ya Shilingi 110 kwa kila hisa inayolipwa kikamilifu wakati wa maombi.

Wanahisa waliopo tu wa DCB Commercial Bank PLC katika tarehe ya rekodi ndio wanaweza kutuma maombi.

### Maelekezo ya Fomu ya Maombi

Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya kabla ya kujaza fomu. Fomu hii inapojazwa kabla ya tarehe ya kufunga, inapaswa kuwasilishwa kwa mshauri wa miamala kwa kujaza fomu iliyo hapa chini au kutumia fomu ya wavuti iliyoidhinishwa (kiungo hapa chini) au kwa wakala aliyeidhinishwa wa kupokea, kwa anwani iliyosajiliwa ya DCB au kwa tawi la benki inayopokea kabla ya Saa 10:00 jioni siku ya Ijumaa Disemba 6 2024.

Maombi yote lazima yawiane na Jina katika Rekodi ya CSDR. Wakurugenzi wa DCB Commercial Bank PLC wana haki ya kukubali au kukataa maombi yote kwa ujumla au sehemu ikiwa maelekezo yaliyoainishwa katika Dokezo hili hayatafuatwa kikamilifu.

Maombi yote yaliyokubaliwa yatapokea risiti ya amana ya CSD kama uthibitisho wa umiliki wao wa hisa katika DCB. Marejesho yote (ikiwa yapo) yatafanywa kwa Akaunti ya Benki ya wanahisa wenye sifa au kupitia Miamala ya Simu ya Mkononi kama ambavyo mhusika ameelekeza kwenye fomu yake ya maombi.

### TAFADHALI SOMA MWONGOZO WA MAOMBI KABLA YA KUJAZA FOMU HII

| OFA YA MGAO WA MUDA | USTAHIKI WA MWANAHISA |
|---|---|
| Jina au Majina ya Mwanahisa/Jina la Kampuni: | Nambari ya CDS katika Soko la Hisa: |
| Hisa za Kawaida Wakati wa Tarehe ya Kurekodi: | Hisa za Upendeleo: |
| Nambari ya Kitambulisho cha Taifa/Hati ya Kusafiria: (Binafsi) | Namba ya Usajili: (Makumpuni) |

| MAELEZO YA MWANAHISA MWENYE SIFA | |
|---|---|
| Anuani za Kudumu: | Barua Pepe: |
| Nambari ya simu ya Mkononi: | Simu: |
| Jina la Akaunti ya Benki: | Nambari ya Akaunti ya Benki: |
| Jina la Benki: | Tawi la Benki: |

**A. KUSTAHIKI & KUKUBALI**

| UKUBALI KWA UKAMILIFU | KIASI KINACHOLIPWA |
|---|---|
| Mimi/Sisi, tunakubali kuchukua Hisa za Upendeleo zote kwa ukamilifu, kwamba kwa kuzingatia masharti ya Dokezo la DCB la tarehe 11 Novemba 2024 na Mkataba na Nakala za Usajili za DCB Commercial Bank PLC | |

| KUKUBALI KWA SEHEMU TU | KUKUBALI KWA SEHEMU TU | KIASI KINACHOLIPWA |
|---|---|---|
| Mimi/sisi tunakubali kwa sehemu kuchukua Hisa za Upendeleo, kwamba; kwa kuzingatia masharti ya Dokezo la DCB la tarehe 11 Novemba 2024, PAO hii na Mkataba na Vifungu vya Usajili wa DCB Commercial Bank PLC. | | |

**B. MAOMBI YA HISA NYONGEZA IWAPO ZITAPATIKANA**

Wanahisa wanaruhusiwa kutuma maombi ya hisa za ziada iwapo zitakuwepo:

| KUKUBALI KUCHUKUA HISA ZA ZIADA | IDADI YA HISA | KIASI CHA KULIPIWA |
|---|---|---|
| Mimi/Sisi, Tunaleta maombi ya hisa za ziada iwapo zitakuwepo, kwa mujibu wa masharti ya Dokezo la DCB la tarehe 11 Novemba 2024 na Mkataba na Hati za Usajili za DCB Commercial Bank PLC. | | |
| **IDADI YA JUMLA INAYOOMBWA (A+B)** | | |

## C. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Tafadhali hakikisha unatumia Nambari yako ya CDS kama rejea ya uhamishaji wowote wa Malipo unaofanywa na TISS/Amana ya moja kwa moja au Uhamisho wa Pesa kwa Simu ya Mkononi.

### 1: KWA NJIA YA BENKI

BENKI INAYOPOKEA (KUPITIA TISS AU KUWEKA KWENYE AKAUNTI)

Jina la Benki: DCB Commercial Bank

| | |
|---|---|
| Jina la Akaunti: | DCB RIGHTS ISSUE COLLECTION ACCOUNT |
| Nambari ya Akaunti: | 22100145 |
| Swift Code: | DASUTZTZ |

### 2: KUPITIA SIMU YA MKONONI

Kwa wanahisa wanaolipa chini ya Shilingi 5,000,000

Hamisha kutoka Simu ya Mkononi kwenda Akaunti ya Benki kwa kufuata taarifa za kibenki kwenye Nambari 1 hapo juu

Zingatia: Ikitokea kuna Kurejeshewa fedha, zitatumwa kwenda Akaunti ya Benki au nambari ya simu ambayo pesa zilipokelewa.

## D. KWA WAKURUGENZI WA DCB COMMERCIAL BANK PLC

Mimi/Sisi, tuliotia saini hapa chini, tunathibitisha kwamba baada ya kusoma Dokezo hili na kwa kuwa Mwanahisa mwenye sifa wa DCB Commercial Bank Plc, tunatuma maombi bila kubatilishwa na kuomba kukubali ombi lililo hapo juu kama Hisa za Upendeleo ya kupata hisa pamoja na maombi ya hisa zozote za ziada zilizogawiwa miongoni mwao na ambazo hazijachukuliwa kwa bei ya Shilingi 110 kwa kila hisa kwa kufuata masharti yaliyotolewa kwenye Dokezo, na kwa kuzingatia masharti ya DCB Commercial Bank Plc.

Nina/Tunaambatisha uthibitisho wa malipo kulingana na Kifungu C cha fomu hii kwa ajili ya Toleo la Hisa za Upendeleo ya kupata hisa za DCB Commercial Bank Plc.kwa kiasi kinachofaa kulingana na masharti ya maombi haya.

| Jina la Mwombaji | Saini/Muhuri wa Kampuni Inayoomba |
|---|---|
| ______________________ | ______________________ |
| ______________________ | ______________________ |

**Mshauri Kiongozi na Dalali Mdhamini**


iTrust FINANCE

Trust Finance Limited

Block C, Plot No. 429, Mahando St Po. Box 22636, Masaki

Dar es Salaam, Tanzania

Stockbrokers | Fund Managers | Investment Advisors



DCB COMMERCIAL BANK



Makao Makuu, Jengo la DCB,
Magomeni Mwembechai,
Kiwanja Na. 123 Kitalu R, Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 19798, Dar es Salaam,
Simu ya Mkononi: +255 713 986 686,
Simu: +255 222 172 201,
Faksi: +255 22 2172201